# Mwongozo wa mwalimu

## Wakati wa biblia Kiwango 3 na 4

Msururu A

Masomo 7 - 12

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)

**Misheni yetu**

Kutunga mafundisho ya Biblia kwa walimu ili wafundishe ukweli wa Yesu Kristo kwa kizazi kinachokuja katika dunia yote.

**Maono yetu**

Kufikia kizazi kinachokuja na ufahamu wetu wote katika lugha zao kwa kuendeleza na kusaidia shirika la kimataifa la washiriki waliojitolea.

## HABARI KWA JUMLA

**Kazi inayofanywa na Bible Educational Service:**

Kazi ya mafundisho ya kibiblia (Bible Educational service) inachapisha katika kingereza mafundisho ya Biblia “Bibletime”’, “New Life” na “Gleaner”. Inasaidia vituo vya usambazaji wa mafundisho hii na kila shirika ya namna hiyo inayozitumia katika Uingereza na pahali pengine duniani, kwa njia ya kuwatembelea, kuwashauri, na wakati wa kuwafundisha. Katika inchi mbalimbali, Bes iliendeleza pia ushirikiano na vikundi nyingi vinavyofanya kazi ya utafsiri, muundo, uchapishaji na usambazaji wa mafundisho. Kila mara inapewa bure kwa wote.

Mafundisho “wakati wa biblia” ilianza pale Irland tangu miaka zaidi ya 50. BES iko na hati miliki ya mafundisho katika kiingereza vilevile katika lugha zote zingine. Sehemu kubwa ya mafundisho hii imechapishwa katika muundo wa A4 na inatumiwa kama mafundisho kwa mfano wa barua katika inchi nyingi zinazozungumza Kiingereza. Kama inajazwa na watoto, masomo inarudishwa, baada ya kila wiki ine, katika kituo kimoja ili ipewe pointi (Bible school Center). Tangu muda mfupi, mafundisho imechapishwa pia katika vitabu vya muundo wa A5, vilivyo na mafundisho ya miezi sita, kupitia Revival Movement katika Irland ya kaskazini. Hii iliwezesha kabisa utumizi wake katika ma kanisa na shule, zaidi katika eneo ambako kazi ya posta haipo tena.

Mafundisho ya BES inapatana pia vema na utumizi wa kibinafsi nyumbani ao katika kundi, ikiwa ndani ya ma kanisa ao ndani ya ma shule. Programu iliyotungwa inawezesha watoto na vijana kuendelea kujifunza Biblia muda wa zaidi ya miaka kumi. Viwango tano vya masomo vinapatikana sasa katika kiingereza (miaka 3 - 4, miaka 5 – 7, miaka 8 - 10, miaka 11 – 13, miaka 14 – 16). Kwa kila mmoja wao, programu inachukua miaka tatu. Mtoto ao kijana anaweza kujifunza viwango tofauti kulingana na uwezaji wake kibinafsi. “Wakati wa biblia” inaleta kwa watoto na vijana nafasi kwa kujifunza Neno la Mungu, kujifunza hadisi za Biblia na kuelewa maana ya injili katika maisha yao wenyewe.

Mafundisho inayopatikana katika ufaransa inaweza kuchapishwa kutoka tovu – www.besweb.com – ao kwa kumuomba katibu wa kimataifa. Inapatikana pia kwa lugha zingine katika tovu. Pia kuna vitabu vingine ambavyo vinaweza kuwa vya muhimu kwa inchi mpya ao maeneo inayotaka kuanzisha kituo cha BES.

## Anuani ya kufaa:

**UK (Northern Ireland) Office (ghala za masomo zote)**
Bw. Samuel Balmer
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Phone: 0286 632 2462

Site web: www.besweb.com
Email: info@besweb.com

## MWONGOZO WA MWALIMU

Katika mwanzo, mafundisho ya "Wakati wa Biblia" ilitolewa kwa mfano wa mafundisho kwa njia za barua kwa ushirikiano na kituo kimoja cha "shule ya Biblia kwa njia ya posta". Lakini, zaidi na zaidi mafundisho hii inasomwa pahali ambapo kazi ya posta siyo ya kuaminika, hasa katika shule na ma kanisa katika Afrika, India na pahali pengine. Mwongozo wa mwalimu uko pale kwa kusaidia wale wanaotumia mafundisho katika mazingira kama haya. Kitabu hiki kinatungwa juu ya kuwa mwongozo wa kiwango 3 na 4, ambavyo vinakusudiwa watoto kutoka umri wa miaka 11 hadi 16.

Maelezo ya mwongozo huu yanafuata maandiko ya Biblia ambayo ni namna moja na ile iliyo katika mafundisho yenyewe. Mafundisho, na maelezo, imetungwa mu namna ya somo moja kwa wiki. Kwa hiyo, masomo katika Aprili inaambatana na Pasaka na masomo katika Desemba inaambatana na Krismasi.

Kulingana na pahali, ao masomo kwa wiki katika muundo wa A4, ao vitabu vya muundo wa A5 ambamo muna masomo 24 kwa miezi 6, vitatumiwa. Ni mwalimu ndiye atagawa masomo A4 kwa mwezi. Kila wiki karatasi itajazwa kwenye kanisa ao shule, ao itapelekwa kwa mtoto na kurudishwa yenye kujazwa, baada ya wiki moja. Mwisho wa kila mwezi, mwalimu atachukua masomo na ataipatia ma pointi; atairudisha kwa wanafunzi yenye kurekebisha, kwa haraka iwezekanayo.

Kitu kizuri ni kwamba, vitabu vya muundo wa A5 vinapaswa kuchukuliwa na kupewa ma pointi mwisho wa kila mkutano, lakini mara nyingi tunaona kwamba haiwezekane. Katika kesi hii, ni vema kuigawa kwa wanafunzi wengine, na mwalimu ataleta ma pointi kwa masomo akisema kwa sauti na wakati wanafunzi watakuwa wanarekebisha na kuweka alama katika masomo ya wenzao. Katika ukurasa wa mwisho wa kila kitabu, kuna pahali ambapo inaruhusu kuandika kiwango cha kufaulu cha kila mwezi, na pia maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Kwenye cheti hiki inaonekana nambari ya kiwango cha kufaulu kwa mwanafunzi muda wa miezi sita ya masomo.

## MASHAURI YA MUHIMU KWA WALIMU

Hapa, lengo siyo kwamba ni maagizo kwa walimu na kuwanyima uwezekano wote wa kulinganisha somo, kufuatana na mawazo na mipango yao wenyewe. Ni mapendekezo tu ambayo inaweza kusaidia katika utumizi wa mafundisho ya "wakati wa Biblia".

- **Kujua historia vizuri –** Mwalimu anapaswa kufanya yote iwezekanayo ili ajue vizuri historia ya Biblia, vilevile mafundisho ya  "wakati wa Biblia" ambayo inaambatana nayo. Iliyo vema ni kwamba amalize yeye mwenyewe kujifunza somo kabla ya kuwaambia watoto. Maelezo ya mwongozo inapaswa pia kusomwa na uangalifu kwa kusaidia katika kupangwa kwa kila somo.
- **Kuelewa mafundisho ya kushika –** Juu ya kila ukurasa, unaweza kusoma: "tunajifunza kwamba", inafuatiwa na nukta mbili kubwa ambayo tunatumaini kwamba watoto wataelewa kisha kusikia maelezo ya mwalimu na kisha kujifunza mafundisho ya  "wakati wa biblia". Nukta kubwa ya kwanza inaelekea ufahamu na uelewa wa historia. Ya pili inatia watoto moyo kwa kushika kibinafsi mafundisho inayopatikana katika historia hiyo. Ma nukta kubwa hii ya kushika inafanya muhtasari wa ukweli muhimu ambao ulifundishwa katika somo. Mwalimu anaweza kuitumia kwa "kujipima kibinafsi" kutokana na mafundisho iliyopewa, pia uelewa wa watoto.
- **Kutanguliza –** Mafundisho yote inaanza kwa kuambatanishwa na mambo ambayo watoto wenyewe waliishi, inayofanana na jambo ambayo inaelezwa katika historia. Mawazo mengi yamependekezwa juu ya kutanguliza hadisi na kuwezesha watoto wajifunze kwa bidii tangu mwanzo wa huu wakati wa mafundisho ya Biblia.
- **Kufundisha –** Ma nukta kubwa za historia zimetajwa. Tunatumaini kwamba mwalimu hatakuwa anaisoma wakati anaieleza. Lakini, lazima ajue vizuri historia ili aweze kuisema kwa bidii na kuamsha akili. Atafanya kwamba wanafunzi waelewe mafundisho kubwa ya kushika na atawaongoza katika jinsi wanaweza kujibu na kuitumia. Tulijaribu, ilivyowezekana mara kwa mara kutoa maelezo fulani wakati historia inapoelezwa. Hiyo inaonekana kila mara katika maandishi ya *italiki*.
- **Kujifunza –** Kila historia inaambatana na shairi muhimu. Wakati mwingine kuna mbili, kama ya pili iliongezwa, inaweza kuwa mwepesi kukamata katika akili. Tunatumaini kwamba watoto watajifunza vizuri ma shairi muhimu na mara kwa mara watakuwa na nafasi kwa kuirudia juu ya kuikumbuka vema.
- **Kujaza somo –** Ikiwa masomo inafundishwa katika shule, mwalimu atajua kama watoto wanaweza kujaza masomo pekee ao kama wanahitaji kusaidiwa. Ikiwa ni lazima, inapaswa mwalimu awasomee maandiko ya

somo watoto wengine ambao hawataweza kusoma pekee. Katika kesi moja kama katika nyingine, inaweza kuwa ya mafaa kuamsha akili ya wanafunzi katika ma nukta moja ambayo inapatana na maswali.
Kama mafundisho ya "wakati wa biblia" inatumiwa katika mazingira ingine isiyokuwa shule, ni ya muhimu kwamba mwalimu awe mwema na tayari kusaidia watoto ili mafundisho hii isionekane kuwa kitu cha magumu na cha kuchokesha, lakini kwa tofauti ionekane kuwa wakati wa kufurahisha. Ni ya muhimu pia kuwatia moyo watoto na kuwapongeza wakati wanapojifunza.

- **Kuimarisha** – Mawazo ya kibinafsi ao katika kundi, michezo kidogo imetungwa kwa ajili ya kusaidia majifunzo na marudio ya historia.
- **Kushika –** Katika sehemu hii, changamoto ya kibinafsi imepewa kwa wanafunzi. Mara nyingi, kazi inapewa kwa ajili ya kuongoza wanafunzi kuambatanisha mafundisho na maisha yao ya kila siku.
- **Kuonyesha –** Katika ma kesi nyingine, tunajua kwamba inaweza kuwa magumu kuwa na vyombo vya kuonyesha picha. Lakini ikiwezekana, ni ya muhimu sana kuonyesha picha ao vitu ambavyo vitasaidia watoto kuelewa historia kwa njia ya mifano. Ma picha inaweza kupakuliwa katika tovu www.freebibleimage.org. Eikon Bible Art (www.eikonbibleart.com) inaleta pia vyombo vya kuonyesha picha lakini vifaa vyake ni vya kuuza. Ikiwezekana, mifano iliyo katika mafundisho ya "wakati wa biblia" inaweza kunenepeshwa na fotokopi, kisha kuwekwa rangi na kutumiwa kwa kuonyesha picha.

## Kufundisha mstari muhimu

1) Shairi inaweza kuandikwa katika karatasi kubwa ao katika kibao. Kisha, maneno mengi inaweza kuondoshwa polepole wakati watoto wanatamka shairi, mpaka wakati hakutabaki tena neno hata moja na wafikie kutamka shairi yote mzima, bila kusaidiwa.
2) Kwa kutanguliza mstari muhimu unaweza kutumia:
   a) Mchezo wa kujaza visanduku: Mstari muhimu inaandikwa na herufi nyingi ambazo zinakosekana, hakuna neno inayo herufi zote. Watoto wanapendekeza herufi juu ya kujaza ma tundu, mpaka wakati mmoja wao anatambua shairi.
   b) Kila mtoto ana Biblia na wote wanafukuzia ili wavumbue shairi wa kwanza. Wa kwanza kuipata lazima aisome kwa sauti kubwa.

## Kusimamia muda

- Maelezo yote yameundwa namna moja, ikilinda taratibu moja ya sehemu tofauti. Lakini ikiwa ni lazima, mwalimu anaweza kubadilisha muundo.
  1. Kueleza na kufundisha historia: Karibu dakika 15,
  2. Kujifunza Mstari muhimu: karibu dakika 5 mpaka 10,
  3. Kujaza karatasi: dakika 20,
  4. Michezo na ma kazi nyingine: dakika 5 mpaka 10.

Kumbuka haya:

"Uniambie na naweza kusahau,
Unionyeshe na nitakumbuka,
Unishirikishe na nitaelewa"

## Kitabu cha Wakati wa Biblia

| | Hatua ya 1 (miaka 5-7)<br>Hatua ya 2 (miaka 8-10) | Hatua 3 (miaka 11-13) | Hatua 4 (miaka 14+) |
|---|---|---|---|
| MSURURU A | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Abrahamu<br>6. Abrahamu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa kwanza<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji na kuanguka<br>2. Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya kikristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas |
| MSURURU B | 1. Utoto wa Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Mafumbo<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Yesu anakutana na watu<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Waandishi wa Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Bwana Yesu<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Maisha ya Yosefu<br>8. Njia ya kwenda<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Sheria<br>12. Muujiza wa Krismas |
| MSURURU C | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Historia ya pasaka<br>5. Ruta na Esiteri<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu waliotumiwa na Mungu<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Yesu ine<br>3. Nguvu ya Bwana<br>4. Bwana Yesu<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu wa Agano la Kale<br>12. Kuzaliwa kwa Kristo |

| | A7 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maisha ya Yakobo<br>Kichwa – Mdanganyifu | A7 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Yakobo<br>Kichwa – Mdanganyifu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 25:21-34***<br>**Mstari muhimu:** ***Zaburi 32:1***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anaweza kutusamee wakati tunatenda zambi.<br>2. Mungu anataka kubariki kila mmoja wetu kwa upekee. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 25:19-34; 27:1-41***<br>**Mstari muhimu:** ***Waroma 5:8***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Kudanganya na kusema uwongo vinaleta magumu na ole.<br>2. Mungu ana mpango juu ya maisha ya kila mtu. |
| KUTANGULIZA | Muzungumzie pamoja kuhusu maana ya “majaribu”, na nyakati ile tunajaribiwa kusema uwongo. Fanya daftari ya moja za nyakati hizi na angalia ni kwa nini tunaweza kusema uwongo.<br>Muzungumzie pia kuhusu wivu, nyakati zile tunaweza kupata wivu, na ni kwa sababu ya nini. | Tunapaswa kuishi na matokeo ya matendo yetu. Uiambatanishe na maisha yako mwenyewe. Kwa mfano, kumbuka wakati moja ambao wewe ao mtu ambayo aunajua alipata shida, pengine kwenye polisi kwa sababu ya udanganyifu ao uwongo. Muwaze pamoja kwa nini kuvunja sheria (zambi) inapaswa kuapizwa. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Kisha maombi ya Isaka, Rebeka amezaa mapacha, wa kwanza Esau na mdogo Yakobo.<br>2. Kuna upendeleo katika familia hii; Isaka anampenda Esau mwindaji, lakini Rebeka anampenda Yakobo ambaye anapenda sana kubaki nyumbani.<br>3. *Eleza umuhimu wa haki ya mzaliwa wa kwanza katika mashariki ya zamani.*<br>4. Esau anawinda na ana njaa; Yakobo anapika supu lakini atampa ndugu yake ila tu akimuuza haki ya mzaliwa wa kwanza.<br>5. Isaka ambaye amezeka, anataka kumbariki mwana wake mzaliwa wa kwanza, lakini Rebeka na Yakobo wamefanya shauri ili wamdanganye Isaka ambaye haoni tena. Wakati Esau alipoenda kuwinda nyama ili ampikie baba yake chakula, Rebeka na Yakobo wanapika chakula kwa haraka, kisha Rebeka amemfanya Yakobo aonekane kama ni mwingine na anamwambia baba yake kwamba yeye ni Esau. Hivi, amepata baraka ambayo iliwekewa mwana mzaliwa wa kwanza.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Kisha maombi ya Isaka, Rebeka amezaa mapacha, wa kwanza Esau na mdogo Yakobo.<br>2. Kuna upendeleo katika familia hii; Isaka anampenda Esau mwindaji, lakini Rebeka anampenda Yakobo ambaye anapenda sana kubaki nyumbani.<br>3. *Eleza umuhimu wa haki ya mzaliwa wa kwanza katika mashariki ya zamani.*<br>4. Esau anawinda na ana njaa; Yakobo anapika supu lakini atampa ndugu yake ila tu akimuuza haki ya mzaliwa wa kwanza.<br>5. Isaka ambaye amezeka, anataka kumbariki mwana wake mzaliwa wa kwanza, lakini Rebeka na Yakobo wamefanya shauri ili wamdanganye Isaka ambaye haoni tena. Wakati Esau alipoenda kuwinda nyama ili ampikie baba yake chakula, Rebeka na Yakobo wanapika chakula kwa haraka, kisha Rebeka amemfanya Yakobo aonekane kama ni mwingine na anamwambia baba yake kwamba yeye ni Esau. Hivi, amepata baraka ambayo iliwekewa mwana mzaliwa wa kwanza.<br>6. *Zungumzeni pamoja kuhusu huu mfano wa udanganyifu kisha eleza jinsi ni ya muhimu kuwa mwenye haki.*<br>7. Wakati Esau aliporudi, alikasirika na kumsihi baba yake ampe baraka, lakini imekuwa nyuma kabisa. Amepoteza haki yake ya muzaliwa wa kwanza pia baraka.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| KUIMARISHA | Waza kuhusu zambi ambayo Yakobo alitenda katika somo hii. Sisi tunahitaji usamee juu ya zambi ya namna gani? Zungumzieni pamoja, kisha chukueni muda kidogo kwa kufikili kibinafsi.<br>Andika majibu ya wanafunzi katika kibao kwa mpangilio usio sawa. Muchunguze jinsi tunaweza kumuomba Mungu usamee, pia watu wengine. Soma ***Zaburi 32:1-5*** kwa kukusaidia. | Waza jinsi Esau alijisikia wakati alipotambua udanganyifu na uwongo wa ndugu yake na mama yake.<br>Kumbuka nyakati ulipata magumu kwa sababu ulisema uwongo ao ulidanganya na Andika vitu mbili kwa upekee ambavyo utajaribu kutumia na nia ya kutafuta kuishi mu namna ingine tangu sasa. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Andika katika karatasi moja zambi fulani ambayo ulifanya, kisha uipasue kwenye yalala. Ao, Andika zambi fulani katika mchanga ao katika udongo wenye vumbi kisha uifute. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Chunguza mipango ya Mungu juu ya Yakobo na anaweza kuwa nayo juu yako, kulingana na kanuni za kibiblia iliyo katika ***Yeremia 29:11.***<br>2. Omba Mungu akufunulie mambo zaidi kuhusu maisha yako ya siku zijazo. Uwe na nia nzuri! |

| | A7 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maisha ya Yakobo<br>Kichwa – Mlotaji | A7 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Yakobo<br>Kichwa – Mlotaji |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 27:41-46; 28:10-22***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 28:16***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Hata kama Yakobo alifanya tendo mbaya, kila mara Mungu alikuwa naye na alimpenda sana.<br>2. Ni namna moja kwetu sisi pia. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 27:41-46; 28:10-22***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 28:16***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Hata kama Yakobo alifanya tendo mbaya, alikutana na Mungu mu namna ya kipekee, ambaye alimupa ahadi nzuri.<br>2. Kila mara Mungu anatutendea kama alivyofanya na Yakobo. |
| KUTANGULIZA | Fikirieni kuhusu jinsi Mungu anaongoza maisha yetu, ingawa chochote tunachofanya! Fikirieni njia tofauti za mawasiliano ambayo tunayo pia jueni kwamba Mungu vilevile anaweza kusema nasi mu namna tofauti. Uliza wanafunzi waseme ni njia gani ambazo Mungu anaweza kutumia kwa kusema nasi wakati wa sasa? | Ambia wanafunzi waeleze historia ya wakati fulani ambao mtu moja ambaye alimtumainia Mungu na aliishi mambo ya ajabu, isiyo ya kawaida.<br>Inatupaswa kuwa wakamilifu ili tuishi mambo ya namna hii? |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Esau anawaza jinsi anaweza kumuua Yakobo baada ya kufa kwa baba yake. Rebeka analeta wazo ya kwamba Yakobo aende kuishi kwa mjomba yake Labani mpaka hasira ya Esau itakapotulia.<br>2. Isaka anambariki Yakobo naye anaenda katika Padani-Aramu.<br>3. Yakobo anasimama usiku na analota ndoto. Anaona kipandio kinagusa mbinguni. Kisha Bwana anasema naye na anampa ahadi kuhusu inchi ambayo familia yake itapata kama uriti. Anaahidi pia Kwenda naye pamoja katika safari yake yote.<br>4. Yakobo ameamka na anaita pahali pale kwa jina la Beteli, maana yake nyumba ya Mungu.<br>5. Yakobo anafanya kiapo: Ikiwa Mungu anamchunga, basi Yakobo atamchagua Mungu huyo kuwa Mungu wake!<br>6. *Chunguza majifunzo ya kupata katika mambo ambayo aliishi pale Beteli.*<br>7. Zungumzieni pamoja kuhusu mapendo ya Mungu kwa ajili ya Yakobo, lakini siyo sababu ya zambi yake.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Esau anawaza jinsi anaweza kumuua Yakobo baada ya kufa kwa baba yake. Rebeka analeta wazo ya kwamba Yakobo aende kuishi kwa mjomba yake Labani mpaka hasira ya Esau itakapotulia.<br>2. Isaka anambariki Yakobo naye anaenda katika Padani-Aramu.<br>3. Yakobo anasimama usiku na analota ndoto. Anaona kipandio kinagusa mbinguni. Kisha Bwana anasema naye na anampa ahadi kuhusu inchi ambayo familia yake itapata kama uriti. Anaahidi pia Kwenda naye pamoja katika safari yake yote.<br>4. Yakobo ameamka na anaita pahali pale kwa jina la Beteli, maana yake nyumba ya Mungu.<br>5. Yakobo anafanya kiapo: Ikiwa Mungu anamchunga, basi Yakobo atamchagua Mungu huyo kuwa Mungu wake!<br>6. *Zungumzieni pamoja kuhusu mapendo ya Mungu kwa ajili ya Yakobo, lakini siyo sababu ya zambi yake.*<br>7. *Fikilieni kuhusu maajabu ambayo inaweza kutunongojea katika maisha yetu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | Fanyeni ma Kundi kidogo. Tajeni pahali ambapo mulisikia uwepo wa Mungu, mukitumia kichwa cha neno "Mungu alikuwa pamoja nami." Fikilieni kuhusu matokeo ya ***Waebrania 13:5*** katika maisha ya kila siku. | Je, Mungu amekwisha kukulotesha ndoto? Umekwisha kupata ndoto ambayo ina maana ya kiroho? Kulingana na wewe, maana yake ilikuwa nini? Ndoto hii ilikuwa na mafaa gani kwako?<br>Chunguza ni ma njia gani kupitia ile Mungu anaweza kusema na watu siku hizi?<br>Ni ahadi gani ambayo Mungu alikufanyia wewe leo kwa upekee? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Umekwisha kuishi wakati moja ambao ulifanya zambi lakini ulijua kwamba Mungu hakukuacha, lakini alikubariki?<br>2. Mambo ya namna hii inaleta Mawazo gani ndani yako?<br>3. Unawaza Mungu angeweza kusema nawe namna gani? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tafuta ndoto za kiroho kisha uwe wazi kwa kile Mungu anasema nawe katika somo hii.<br>2. Tafuta ahadi ine za Mungu katika Biblia. Uitumie katika maombi. |

| | A7 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Maisha ya Yakobo<br>Kichwa – Kukata tamaa | A7 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Yakobo<br>Kichwa – Kukata tamaa |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 29:1-30***<br>**Mstari muhimu:** ***Wagalatia 6:7***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Maisha inafanana na tendo la kupanda na kuvuna.<br>2. Mungu hakuahidi kamwe kwamba maisha itakuwa rahisi. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 29:1-30; 31:1-21***<br>**Mstari muhimu:** ***Wagalatia 6:7***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Maisha inafanana na tendo la kupanda na kuvuna.<br>2. Kitu ambacho Mungu anasema kinapaswa kuhesabiwa kwamba kina heshima, kwa sababu mambo anayosema ni kweli.<br>3. Tunapaswa kuwatendea wengine jinsi tunataka watutendee. |
| KUTANGULIZA | Leta mfano wa kupanda na kuvuna katika bustani, katika shamba, na kazalika; kisha onyesha kwamba mbegu fulani itazaa mavuno fulani. Uifananishe na mwenendo wetu. Iwe mzuri ao mbaya, kila mara kutakuwa matokeo! Tutavuna kile ambacho tulipanda.<br>Taja watu wamoja waliojulikana kabisa ambao walikuwa na mwenendo mbaya na kwa hiyo walipata matokeo. | Leta mfano wa kupanda na kuvuna katika bustani, katika shamba, na kazalika; kisha onyesha kwamba mbegu fulani itazaa mavuno fulani. Uifananishe na mwenendo wetu. Iwe mzuri ao mbaya, kila mara kutakuwa matokeo! Tutavuna kile ambacho tulipanda.<br>Tafuta katika ma gazeti za mtaa, mifano ya kupanda na kuvuna. Fanya vipande vya picha kisha uongeze maneno ya muhimu. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yakobo amefika Padani- Aramu na anakuta wachungaji wanaokunywesha nyama zao.<br>2. Rakeli, dada yake, amekuja pia kwa ajili ya kunywesha nyama zake na Yakobo anamsaidia. Wakati alipomwambia baba yake Labani kwamba Yakobo amekuja, anampokea kwake.<br>3. Yakobo anamtumikia Labani na huyo anamlaka kwamba ikiwa anamtumikia muda wa miaka saba, Yakobo atamuoa Rakeli yule alipenda.<br>4. Siku iliyofuata baada ya ndoa, Yakobo anavumbua kwamba alidanganywa, na amepewa Lea, dada wa Rakeli.<br>5. Baadaye, anampokea Rakeli pia kama mke, lakini alitumika tena miaka saba ya nyongeza kwa ajili yake.<br>6. *Zungumzieni kuhusu jambo la kwamba Yakobo, mdanganyifu, amevuna hapa matokeo ya udanganyifu wake mwenyewe hapo nyumbani.*<br>7. *Zungumzeni pia kuhusu njia tofauti za kutengeneza mambo mbaya katika maisha.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yakobo amefika Padani- Aramu na anakuta wachungaji wanaokunywesha nyama zao.<br>2. Rakeli, dada yake, amekuja pia kwa ajili ya kunywesha nyama zake na Yakobo anamsaidia. Wakati alipomwambia baba yake Labani kwamba Yakobo amekuja, anampokea kwake.<br>3. Yakobo anamtumikia Labani na huyo anamlaka kwamba ikiwa anamtumikia muda wa miaka saba, Yakobo atamuoa Rakeli yule alipenda<br>4. Siku iliyofuata baada ya ndoa, Yakobo anavumbua kwamba alidanganywa, na amepewa Lea, dada wa Rakeli<br>5. Baadaye, amempokea pia Rakeli kama mke, lakini alitumika tena miaka saba ya nyongeza kwa ajili yake.<br>6. *Zungumzieni kuhusu jambo la kwamba Yakobo, mdanganyifu, amevuna hapa matokeo ya udanganyifu wake mwenyewe hapo nyumbani.*<br>7. Baadaye, Mungu anamwambia Yakobo arudi kwenye inchi yake ya kuzaliwa. Mungu alimbariki kwa kumpa wanyama wengi na familia kubwa. Yakobo hakumuambie Labani habari ya Kwenda kwake, lakini anakimbia wakati Labani hayuko nyumbani.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| KUIMARISHA | Fanya ma Kundi kidogo. Kila Kundi itachagua na itaeleza kuhusu jambo moja kati ya mifano ambayo imepewa katika pointi ya 7. Kisha kila Kundi itaweza kuandika mfano “wake” katika kibao ao katika katarasi kubwa, ili mifano yote iweze kuonekana. | Fikilieni kuhusu mifano ya “kupanda” na ya “kuvuna” katika maisha, kwanza mu namna ya mubaya, kisha mu namna muzuri. Andika ao chora majibu yako, ukijaribu kuleta mbili kwa kila mfano. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kumbuka mara ya mwisho ambapo ulikata tamaa.<br>2. Ulitengeneza mambo ile namna gani?<br>3. Ungeweza kuitengeneza mu namna iliyo muzuri zaidi?<br>4. Gawanya katika mistari mbili, unaweza kuleta mifano mbili ya “kupanda” na ya “kuvuna?” | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Unajua mdanganyifu fulani ambaye alidanganywa pia?<br>2. Unaweza kukumbuka mifano ingine mule mwenendo fulani wa kipekee ulio mbaya unarudi kwa kumshika yule mtu? |

| | A7 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maisha ya Yakobo<br>Kichwa – Kuvumbua | A7 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Yakobo<br>Kichwa – Kuvumbua |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 32:1-21; 33:1-11***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Yoane 1:9***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Kwa msaada wa Mungu inawezekana kusamee wengine, hata juu ya vitu vibaya ambavyo walitutendea, kama vile ilifanyika katika maisha ya Yakobo.<br>2. Kila mara Mungu anatusamee wakati tunatubu (tunahuzunika kwa sababu ya zambi zetu) na kumwomba atusamee. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 32:1-2; 33:1-17***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Yoane 1:9***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yakobo alifika wakati wa muhimu kabisa katika maisha yake. Lakini, ni ya muhimu kwake kukutana na Mungu kuliko kukutana na ndugu yake ambaye alihuwa mwenye kusahauliwa tangu muda mrefu.<br>2. Ingawa Yakobo amekomea, Mungu angali na mipango mipya kwa ajili yake. |
| **KUTANGULIZA** | Uwakumbushe watoto kwamba Yakobo anamtii Mungu na kurudi katika inchi yake. Lakini eko na wasiwasi kuhusu kukutana kwake na Esau ambaye alitaka kumuua, miaka iliyopita. Unawaza kwamba Esau atakuwa tayari kumsamee? Fanyeni pamoja daftari ya mambo inayofanyika kwa kawaida:<br>a) wakati wewe hausamee<br>b) wakati wewew hausamee? | Zungumzieni kuhusu mambo yote inayopitikana wakati wa kukutana na mtu wa muhimu sana, na jinsi unaweza kujitayarisha kwa ajili ya ile. Baada ya miaka bila kuwasiliana na Mungu, Yakobo anakutana naye tena. Hiyo ilimbadilisha kabisa, na anapata msaada kwa kukutana kwake na Esau ambako kunakaribia. Ikiwezekana, tafuta katika mtandao “The end of the spear” ao angalia katika DVD sehemu ya filamu mule mjane wa Jim Eliot anasamee watu ambao walimuua mume wake. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Fikiria sababu zinazofanya kwamba Yakobo aogope kurudi baada ya miaka mingi.<br>2. Woga wa Yakobo unaongezeka wakati anajulishwa kwamba Esau anakuja kukutana naye na watu 400.<br>3. Sasa Yakobo anafanya vitu tatu:<br>a) Anagawanya familia yake katika kambi mbili, akitumaini kwamba moja inaweza kuhepuka ***32:8-9***);<br>b) anaomba ***(32:10-13)***<br>c) anamtumia Esau zawadi<br>4. Usiku ule, Yakobo anaishi mambo ya kipekee kabisa. Anakutana na Mungu na aanatafuta baraka yake ***(32:22-31)***.<br>5. Woga wa Yakobo hauko wa maana. Esau anamkaribisha kwa furaha na inaonekana kwamba alimsamee. Yakobo anamuonyesha familia yake na anamsii Esau aitike zawadi yake.<br>6. Ingawa mambo haya yote, asirudi kwa baba yake na anamdanganya Esau mara tena kwani asirudi moja kwa moja.<br>7. *Fikiria kwa nini Yakobo alikuwa na mashaka na hakutumainia ahadi za Mungu.*<br>8. *Eleza woga wako kisha fasilia kwamba woga nyingi haifikie ku kitu hata moja, hata kama tunapitiza wakati nyingi tukiikumbuka katika akili yetu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Fikiria sababu zinazofanya kwamba Yakobo aogope kurudi baada ya miaka mingi.<br>2. Woga wa Yakobo unaongezeka wakati anajulishwa kwamba Esau anakuja kukutana naye na watu 400.<br>3. Sasa Yakobo anafanya vitu tatu:<br>a) Anagawanya familia yake katika kambi mbili, akitumaini kwamba moja inaweza kuhepuka ***32:8-9***);<br>b) anaomba ***(32:10-13)***<br>c) anamtumia Esau zawadi<br>4. Usiku ule, Yakobo anaishi mambo ya kipekee kabisa. Anakutana na Mungu na aanatafuta baraka yake ***(32:22-31)***.<br>5. Woga wa Yakobo hauko wa maana. Esau anamkaribisha kwa furaha na inaonekana kwamba alimsamee. Yakobo anamuonyesha familia yake na anamsii Esau aitike zawadi yake.<br>6. Ingawa mambo haya yote, asirudi kwa baba yake na anamdanganya Esau mara tena kwani asirudi moja kwa moja.<br>7. *Fikiria kwa nini Yakobo alikuwa na mashaka na hakutumainia ahadi za Mungu.*<br>8. Zungumzieni historia ya kweli mule watu walisamee wengine.<br>9. *Fikirieni mabaya ambayo tunajitendea sisi wenyewe pia wengine wakati tunakataa kusamee.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| **KUIMARISHA** | Tumia mawazo ambayo inapatikana katika sehemu iliyo hapa juu ili umwandikie Mungu barua. Uwaulize Watoto ni nini ambayo wanaweza kukiri kwa Mungu, kile wanaweza kumuomba, na kwa sababu gani wanaweza kumshukuru. | Fikirieni kuhu maana ya kukutana na Mungu.<br>a) Inaweza kufanyika wakati gani?<br>b) Inaweza kufanyika namna gani?<br>c) Kwa nini inaweza kufanyika?<br>Uwaulize wanafunzi kama wamekwisha kukutana na Mungu kibinafsi. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Ni kitu gani ambacho tunaweza kujifunza katika hii maandiko ya Biblia kinachoambatana na maisha yetu?<br>2. Leta mifano ya watu ambao walisameewa sasa tu.<br>3. Tunaweza kuomba msaada wa Mungu ili kusamee mtu fulani? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Uwaulize watoto kama hivi karibuni walipata mtu ambaye alikataa kuwasamee, ao mtu ambaye aliwasamee.<br>2. Walijisikia namna gani kwa sababu ya hiyo?<br>3. Kuna mtu ambaye wamepaswa kumsamee. |

| | A8 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maombi<br>Kichwa – Maombi ni nini ? | A8 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Kuwa mkristo<br>Kichwa – Maombi |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Zaburi 5:1-9***<br>**Mstari muhimu:** ***Zaburi 5:3***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Maombi ni kitu moja cha ajabu kwa sababu Mungu mwenyewe ni wa ajabu.<br>2. Maombi ni kuzungumza na Mungu na kumsikia.<br>3. Wakati mwingine hatupate jibu ya maombi yetu na kuna ma sababu juu kwa ile. | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 11:1-10***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 11:9***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Tunapaswa kutambua kwamba maombi ni bahati kubwa.<br>2. Tunapaswa kuomba mara kwa mara.<br>3. Haipaswe kutafuta watu watuangalie wakati tunapofanya maombi ya kibinafsi. |
| KUTANGULIZA | Waza magumu iwezekanayo ikiwa unapaswa kujaribu kupatana na marafiki ao memba za familia walio mbali. Waza kwanza jambo hii ya ajabu: Tunaweza kuzungumza na Mungu.<br>Uwaulize wanafunzi kama weko na zoezo ya kuomba. Kwa nini ndio / Kwa nini hapana? | Waza magumu iwezekanayo ikiwa unapaswa kujaribu kupatana na marafiki ao memba za familia walio mbali. Waza kwanza jambo hii ya ajabu: Tunaweza kuzungumza na Mungu.<br>Uwaulize Watoto kama wemekwisha kupata majibu ya maombi yao. Walifanya nini wakati Mungu aliwajibu? |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Fikirieni kuhusu ni nani tunayesema naye wakati tunaomba maombi yetu kisha fasilia ma cheo ambayo Daudi anatumia katika Zaburi hii.<br>2. Daudi aliomba wakati gani katika mchana? Na sisi, tunaweza kuomba wakati gani?<br>3. Katika Zaburi, vumbua ni nini ambayo inaweza kumzuiza Mungu kujibu maombi yetu?<br>4. Pia, tafuta katika zaburi mafundisho yaliyomo kwa kutusaidia kujitayarisha kwa ajili ya maombi.<br>5. Daudi alikuwa na uhusiano mzuri sana na Bwana hata anamwita kwamba ni “Mfalme wangu na Mungu wangu” katika mstari wa 3. Sisi pia, namna gani tunaweza kuwa na huu uhusiano wa kipekee?<br>6. *Eleza umuhimu wa maombi. Zungumzieni jambo hii. Kwa mfano, maisha ingekuwa jee pasipo maombi?*<br>7. *Tunaweza kuombea mahitaji gani.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Siku moja, Yesu aliomba na wanafunzi wake walimuomba awafundishe jinsi ya kuomba.<br>2. Angalieni ni nani ambaye tunasema naye wakati tunapoomba pia fikilini kuhusu ma cheo mabayo Yesu anatumia katika maombi yake.<br>3. Yesu alianza mfano huu wa maombi na shukrani kwa Mungu. Ni sehemu gani, tunapaswa kuleta ku mashukuru katika maombi yetu?<br>4. Ni mahitaji gani kubwa iliyo katika maombi ya Yesu?<br>5. Soma mfano ambao Yesu alileta kisha ***(Luka 11:5-10)*** kisha fikilieni kuhusu jambo kubwa ya mafundisho ya Yesu: kudumu katika maombi.<br>6. Fikilieni kuhusu mafundisho ambayo Yesu alifundisha ndani ya maombi katika ***Matayo 6:5-15***.<br>7. *Kwako wewe, kwa nini tunaomba zaidi wakati wa magumu?*<br>8. *Tafuteni pamoja ma sababu ambayo inafanya kwamba wakati mwingine tunshindwa kuomba.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| KUIMARISHA | Kuna watu pia mambo ambayo inahitaji maombi yetu?<br>Tunapaswa kuomba mara ngapi? Na kwa muda gani?<br>Fikilieni kuhusu maombi ya mtu mwingine ndani ya Biblia pia kitu tunaweza kujifunza katika mfano wake. | Zungumzieni kwa ufupi kuhusu nukta tano ambayo imetajwa katika majifunzo ya 1 kisha uwaambie wanafunzi wafanye kazi ndani ya vikundi ili watayarishe maombi ambayop ina nukta hizi tano. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Wakati unapoomba, inapaswa kusema zaidi ao kusikia zaidi? Pengine ni muzuri zaidi kusikia kile Mungu anataka kutuambia wakati tunapoomba. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Kumbukeni mambo inayofanyika ndani ya familia, ya jamii, ya inchi. Musisahau kushukuru kwa, ajili ya maombi ambayo imekwisha kupata jibu. |

| | A8 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maombi<br>Kichwa – Mungu anasikia maombi yetu ? | A8 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Kuwa mkristo<br>Kichwa – Kujifunza kuhusu Biblia |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 18:9-14***<br>**Mstari muhimu:** ***Yakobo 4:6***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Hatuhitaji Kwenda kanisani juu ya kuomba: Tunaweza kuomba pahali pote pia wakati wote.<br>2. Mungu anataka kwamba tuwe wenye haki pia waaminifu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 17:10-14; 2 Timoteo 3:14-17***<br>**Mstari muhimu:** ***Zaburi 119:105***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ni ya muhimu kusoma Biblia.<br>2. Ninaweza kwamini Biblia kwa sababu ni Neno la Mungu. |
| **KUTANGULIZA** | Rudieni katika majifunzo ambayo mulipata ndani ya ma somo kuhusu maombi katika Somo 1. Biblia inasema: "… majivuno yanatangulia uharibifu." ***(Mezali 16:18)***<br>Chunguzeni maana yake. Tafuteni mfano moja katika historia ya kweli ao ya mawazo tu. | Duniani kuna Biblia nyingi zaidi ya vitabu vingine vyote. Katika historia, ndani ya inchi zingine, walitafuta kukataza, kuchoma, ao kuzika Biblia, lakini haikuweza kamwe kupotea. Ni kwa sababu ni Neno la Mungu. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu alifundisha kwamba inapaswa kuomba kila mara pasipo kuchoka ***(Luka 18:1)***.<br>2. Alieleza pia kwamba wenye kiburi na kukosa unyenyekevu hawana na nia nzuri wakati wa kuomba.<br>3. Tafuta ni mara ngapi mtu yule mwenye kiburi (mfarisayo) alisema "mimi".<br>4. Uwaulize wanafunzi wafasilie maombi na hali ya mtoza kodi.<br>5. *Onyesha wazi tofauti iliyo katika jinsi ya kuomba ya hawa watu wawili.*<br>6. *Onyesha ni nani ambaye alimpendeza Mungu kati ya hawa wawili na ni kwa sababu ya nini.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Kwa Mkristo, Biblia ndiyo, kitabu cha muhimu sana zaidi ya vyote. Lakini tutasadiki namna gani kwamba ni kweli?<br>2. Katika usomaji wa Biblia tunaona kwamba kila andiko limepewa kwa maongozi ya Mungu, na hiyo inamaanisha kwamba yeye mwenyewe alipulizia "Maneno". Mungu hawezi kusema uwongo na kwa hiyo tunajua kwamba Biblia ni kweli.<br>3. Mambo mengi yalitabiriwa katika Agano la Kale na yalifanyika kweli, wakati mwingine ma mia za miaka baadaye. Kwa mfano kumbuka mifano ya Agano la Kale kuhusu kuzaliwa kwa Yesu.<br>4. Karibu watu 40 waliandika vitabu vya Biblia, muda wa mia nyingi za miaka. Lakini kuna kichwa moja cha neno na ujumbe kubwa ambavyo vinaleta umoja wa kitabu kwa jumla.<br>5. Usomaji wa Biblia na kutii maagizo yake, kwa usaidizi wa Roho Mtakatifu, inaweza kubadilisha maisha ya watu.<br>6. Siyo kitu cha kushangaza kama Biblia ni ya muhimu sana! Fikirieni sababu zote juu yake tunapaswa kuisoma.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| **KUIMARISHA** | Katika karatasi moja, Andika hali ya mtoza kodi, pia katika ingine, hali ya mfarisayo. | Chunguza mstari muhimu na kisha chora nuru ndani ya mbingu. Unaweza kuandika chini yake vitu mule unahitaji nuru ya Mungu, kwa mfano uamuzi wa kufanya, ao msaada wakati uko na huzuni. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Maana ya neno "unyenyekevu ni nini" na namna gani tunaweza kuwa wanyenyekevu zaidi? Leta mifano inayoonekana ya unyenyekevu.<br>2. Maana ya neno "kiburi" ni nini, na tunapaswa kufanya nini ili tuwe wasio kiburi zaidi. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Katika Kutenda, unaweza kufanya namna gani ili usomaji wa Biblia uwe rahisi?<br>2. Waza ili uombe Mungu akusaidie kusoma Biblia mara kwa mara, kuielewa vizuri na kuitumia katika maisha yako ya kila siku. |

| | A8 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Maombi<br>Kichwa – Tunapaswa kuomba namna gani | A4 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Kuwa mkristo<br>Kichwa – Kuishi kwa ajili ya Mungu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 6:5-15***<br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 6:8***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Tunapaswa kuomba mara kwa mara, siyo tu wakati tunapata magumu.<br>2. Maombi yetu haipaswe kuwa ya ajabu ao mrefu.<br>3. Ile "Baba yetu" iko pale kwa kutusaidia namna ya kupanga maombi. | **Usomaji wa Biblia:** ***Yoane 15:1-17; Wagalatia 5:22-23***<br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 15:5***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wakristo wanapaswa kumfanana Yesu zaidi.<br>2. Siri ni kuendelea kuambatana naye, kama vile katika mfano wa mzabibu na matawi yake.<br>3. Wakristo wanahitaji "kutakaswa" na Mungu ili wazae matunda zaidi. |
| **KUTANGULIZA** | 1. Fanya muhtasari mfupi wa masomo 1 na 2 na vyote ambavyo mumekwisha kuona kuhusu maombi. Chunguzeni jambo la kwamba watu wengi wana magumu kwa kuomba mara kwa mara.<br>2. Faida ya kuomba kwa sauti kubwa inaweza kuwa nini, kwa kutusaidia kutia mawazo fasi moja.<br>3. Inaweza kuwa ya faida kwandika maombi ili kutusaidia kupata maneno inayofaa? | 1. Fikiria wakristo ambao wanaonyesha tunda la Roho katika maisha yao. Inawezekana jinsi gani kwao?<br>2. Eleza jinsi Mungu anaweza Kutenda katika maisha yako ili aondoshe vitu visivyo vya faida, vibaya, kama vile mlimaji anasafisha matawi ya mti wa mzabibu. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Bwana Yesu alileta mafundisho kuhusu maombi wakati wa hutuba mlimani.<br>2. Eleza kwa nini maombi ni kitu cha ukaribu sana kati yetu na Mungu.<br>3. Eleza kwa nini kurudia rudia tu maombi sio maombi ya kweli .<br>4. Zungumzeni kuhusu kuhusu faida ya maombi kama kweli Baba anajua mahitaji yetu yote kabla ya sisi kumuomba. (Angalia mstari muhimu).<br>5. Fikirieni kuhusu mfano ambao Yesu ameleta katika ile "Baba yetu" kuhusu mashukuru na mahitaji.<br>6. *Angalieni umuhimu wa kwamini kwamba Mungu atajibu wakati tunapoomba na Kutenda vitu tunavyoomba.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza mfano wa Baba kama mlimaji, Yesu mzabibu, na wakristo, ndio matawi.<br>2. Eleza kwamba Mungu anataka maisha yetu izae matunda, na hiyo imeonyeshwa wazi katika ***Wagalatia 5:22-23.***<br>3. Waza jinsi miti ya matunda iko kabla na baada ya kusafishwa, na kwa nini kusafisha ni lazima kwa ajili ya uzalishaji wa matunda.<br>4. Angalia vizuri tofauti kati ya ***Wagalatia 5:19-20*** pale tunaona matunda ya wanadamu, pasipo usaidizi wa Roho Mtakatifu na pasipo kumwamini Kristo.<br>5. Uwakumbushe Watoto kwamba shabaa ya Mungu, ni kwamba tufanane zaidi na Bwana Yesu, ambaye alionyesha kikamilifu tunda yote ya Roho katika maisha yake.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | Soma ***1 Timoteo 2:1*** kisha zungumzeni kuhusu aina tofauti za maombi yaliyomo.<br>Kumbuka nafasi kwenye tunaweza kuomba kwa upekee. Uiandika wakati wanafunzi wanapoendelea kujibu. | Fanya muhtasari wa mafundisho ambayo unapata katika majifunzo hii.<br>Weka mkazo katika umuhimu wa kukaa ndani ya Kristo kama tunavyosoma katika ***Yoane 15:4-5***. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Maombi siyo kitu cha kufanyiwa na mtu mwingine juu yako; lakini ni kitu ambacho unapaswa kufanya wewe mwenyewe! Waza, hiyo inaweza kumaanisha nini kwako wewe wakati huu?<br>Omba msaada wa Mungu kwa ajili ya kuomba na Imani.Uwatie wanafunzi moyo waandike maombi yao wenyewe, wakibeba mfano wa ile "Baba yetu". | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Uwaambie watoto wasome ***Wagalatia 5:22-23*** katika maombi, ili wamuombe Mungu awaonyeshe ni tunda gani kati ya hiyo, ambayo wanahitaji kuendeleza, kwa usaidizi wake. |

| | A8 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maombi<br>Kichwa – Je, Mungu anajibu maombi ? | A8 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Kuwa mkristo<br>Kichwa – Kumpa Mungu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***1 Samueli 1:1-20***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Samueli 1:20***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu hajibu kila mara maombi yetu jinsi tunataka, ao kwa haraka tunavyotaka.<br>2. Majibu ya Mungu na mipango yetu kila mara ni nzuri zaidi kuliko yetu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Marko 12:41-44; Matayo 6:1-4***<br>**Mstari muhimu:** ***2 Wakorinto 9:7***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Tunapaswa kumpa Mungu kwa furaha. Hiyo ni sehemu ya maisha yetu ya kikristo.<br>2. Kumpa Mungu haikome katika feza. |
| KUTANGULIZA | Umtambulishe Hana na mambo yake.<br>Chora katika kibao picha na misemo ambayo inaonyesha jinsi Hana amejisikia: KABLA YA KUOMBA na BAADA YA KUOMBA. | Katika vikundi kidogo, fanya mbele daftari ya vitu ambavyo Mungu anatupa, kisha daftari ya vitu ambavyo tunaweza kumpa Mungu. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza kwa kifupi mambo ya Hana na familia yake. Eleza pia kwamba kila mwaka walitembelea nyumba ya Bwana na kutoa sadaka.<br>2. Zungumzieni kuhusu jinsi Hana alijisikia kwa sababu hakuwa na mtoto na wakati Penina alikuwa anamchokoza.<br>3. Waza kuhusu maombi ya Hana na ahadi ambayo alimfanyia Mungu.<br>4. Eleza tendo la kuhani Eli wakati alipomuona Hana akiomba.<br>5. Eleza jinsi Mungu alijibu maombi ya Hana.<br>6. Fikirini pamoja kuhusu mabadiliko ambayo yalifanyika katika nia za Hana baada ya kuomba na kumpa Bwana magumu yake.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza mambo iliyofanyika katika hekalu wakati Yesu aliangalia watu wakitoa feza.<br>2. Eleza kwa nini zawadi ya mjane masikini ilikuwa yenye tofauti kabisa na zawadi ya watu wengine.<br>3. Kwa nini amefurahi kabisa kwa ajili ya feza kidogo ambayo mwanamke huyo alitoa?<br>4. Historia hii inatufundisha nini kuhusu kile tunaweza kumpa Mungu? (wakati wetu, vipaji vyetu, mali yetu…)<br>5. Kwa nini Mungu anatuagiza kutoa kwa siri?<br>6. Kumbukeni ahadi ya Mungu kwa wale wanaotoa kwa siri.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | 1. Uwaulize wanafunzi kama wamekwisha kupata huzuni sana kuhusu jambo fulani.<br>2. Tafuteni pamoja nao ni nini wangefanya wakati ule ili wajisikie kuwa na ustarehe.<br>3. Uliza kama kuna mtu ambaye amefarijiwa baada ya kumpa Bwana magumu yake. | 1. Fikirini kuhusu njia nyingi za kumtolea Mungu.<br>2. Chagua nukta moja kwa upekee ambayo itatendeka baada ya majifunzo hii.<br>3. Weka mkazo mbele ya watoto kuhusu umuhimu wa kuwa na msukumo mzuri wakati wanapotoa. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Kumbukeni mtu fulani ambaye anahitaji kujua Mungu anaweza kuchukua magumu yake ili apate ustarehe. Munaweza kumtembelea siku zijazo ili kumwambia hii historia ya Biblia? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Tafuteni mashairi ingine ya Biblia ambayo inasema kuhusu jambo hili. Kwa mfano Yesu alisema “Heri ya kutoa inapita heri ya kupokea” ***(Matendo 20:35)*** Ombeni msaada wa Mungu kwa kuelewa kanuni hii. |

| | A9 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Mtesaji | A9 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Mtume Paulo<br>Kichwa – Kubadilika kwake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 9:1-19***<br>**Mstari muhimu:** ***2 Wakorinto 5:17***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Maisha ya Paulo ilibadilika baada ya kukutana kwake na Kristo.<br>2. Mungu anaendelea kubadilisha maisha leo. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 9:1-31***<br>**Mstari muhimu:** ***2 Wakorinto 5:17***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu pekee ndiye anaweza kubadilisha maisha.<br>2. Kuwa mkristo inaweza kuwa nguvu, lakini Mungu anakaribia watoto wake mu namna ya kipekee kabisa wakati wa magumu. |
| KUTANGULIZA | Umuhesabie Paulo kama mmoja wa wahusika wakuu katika Agano Jipya. Eleza kile alifanya wakati wa kuuawa kwa Stefano ***(Matendo 6:58)***.<br>Beba mfano wa kiwavi anayegeuka kuwa kipepeo kwa kuonyesha nini inafanyika wakati wa kuamini. | Umuhesabie Saulo kama mmoja wa wahusika wakuu katika Agano Jipya. Eleza kile alifanya wakati nwa kuuawa kwa Stefano ***(Matendo 6:58)***.<br>Beba mfano wa kiwavi anayegeuka kuwa kipepeo kwa kuonyesha ni nini inafanyika wakati wa kuamini. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza kwamba Paulo angali na jina yake ya kwanza, Saulo, ambayo alibadilisha baadaye katika historia.<br>2. Eleza sababu ya safari yake kule Damasiki.<br>3. Eleza mambo yote ambayo ilifanyika, na manenambayo ilisemwa wakati Saulo alikutana na Bwana. Maelezo ambayo Paulo alieleza baadaye inaweza kuwa ya mafaa ***(Matendo 22:1-13 na 26:9-18)***.<br>4. Eleza mambo kile kilifanyika wakati alipofika Damasiki na mambo ambayo ilimuongojea.<br>5. Chunguzeni maana ya neno “kubadilika”. Ni kazi ya neema ya Mungu wakati anaumba mtu mpya katika Kristo. Ambatanisha kitu hiki na kuzaliwa mara ya pili ***(Yoane 3:3)***.<br>6. Eleza jinsi Paulo alibadilishwa kisha kukutana kwake na Kristo.<br>7. Weka mkazo katika umuhimu wa ujumbe huu katika imani ya kikristo.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza kwamba Paulo angali na jina yake ya kwanza, Saulo, ambayo alibadilisha baadaye katika historia.<br>2. Eleza sababu ya safari yake kule Damasiki.<br>3. Eleza mambo yote ambayo ilifanyika, na mambo ambayo ilisemwa wakati Saulo alikutana na Bwana. Maelezo ambayo Saulo alieleza baadaye inaweza kuwa ya mafaa ***(Matendo 22:1-13 na 26:9-18)***.<br>4. Eleza mambo kile kilifanyika wakati alipofika Damasiki na mambo ambayo ilimuongojea.<br>5. Kuwa mkristo siyo kitu kiepesi kamwe. Eleza mambo ambayo Saulo alipata kisha tu kukutana kwake na Bwana.<br>6. Angalia kubadilika ni nini: Kazi neema ya Mungu ambaye anaumba mtu mpya katika Kristo. Ambatanisha kitu hiki na ***Yoane 3:3*** na kuzaliwa mara ya pili.<br>7. Kumbuka kwamba Saulo hakugeuke kuwa mtu wa “kidini”; alikuwa vile baada ya y eye kubadilika.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| KUIMARISHA | Fanya kibao moja katika ukuta uandike hapo: “Saulo: kabla na baada”. | Chagua nukta moja kati ya ile mbili iliyo katika sehemu ya “tunajifunza kwamba …” Andika maombi ambayo inaonyesha maana ya hiyo maana ya hiyo katika maisha yako. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Uwasaidie wanafunzi kufikili kibinafsi kuhusu uhusiano wao na Mungu.<br>2. Tunaweza kujifunza nini kuhusu utiifu katika mfano wa Anania? Fanya daftari ya vitu “vya kufanya” kutokana na kile ulijifunza kuhusu utiifu.<br>3. Waza jinsi mkristo anaweza kusaidia mtu mwingine aliye mwamini mpya. Fanya daftari ya njia hizi tofauti pia tafuta Kutenda kabisa vitu ambavyo ulijifunza. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Uwasaidie wanafunzi kufikili kibinafsi kuhusu uhusiano wao na Mungu.<br>2. Waombee Wakristo wanaoteswa leo.<br>3. Soma ***1 Timoteo 1:12-16***. Waza jinsi utazungumzia ***mstari wa 15*** na marafiki wasioamini. |

| | A9 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Magumu | A9 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Mtume Paulo<br>Kichwa – Safari zake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 9:19-30***<br>**Mstari muhimu:** ***Waroma 1:16***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wakati mwingine inaweza kuwa magumu kuishi kama mkristo, kwa sababu si watu wote wanaopenda ujumbe wa Injili.<br>2. Ni ya muhimu kuwatia moyo wakristo wapya. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 11:19-26; 13:1-12***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 13:12***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Kuamini ndio mwanzo wa maisha mapya ndani ya Kristo.<br>2. Ni ya muhimu kufundisha waamini wapya ili wakomee katika uelewa wao wa maisha ya kikristo. |
| KUTANGULIZA | Zungumzeni kuhusu umuhimu wa kutia moyo. Ambia watoto walete mifano ya nyakati ambayo walitiwa moyo, na kueleza kwa nini hiyo ilikuwa ya bei sana kwao. | Kwa njia ya mifano, zungumzeni kuhusu umuhimu wa chakula kwa ajili ya kukomea kwetu kimwili. Ingiza Mawazo ya kukomea kiroho kwa wakristo. Ikiwa muna Biblia pale, ambia mtu moja asome ***1 Petro 2:2 na 2 Petro 3:18***. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Zungumzeni kuhusu mambo ambayo ilifanyika wakati Saulo alianza kuhubiri pale Damasiki, pia eleza ujumbe wake ulitangaza habari gani.<br>2. Eleza jinsi Wayuda walimchukia na namna alivyoweza kukimbia.<br>3. Zungumzeni kuhusu magumu ambayo Saulo alipata. Kwa nini watu walipinga ujumbe wa Injili? Kwa nini Saulo hakuwa na haya juu ya Injili? (Angalia mstari muhimu.)<br>4. Eleza magumu ingine ambayo ilimuongojea Saulo wakati aliporudi Yerusalema.<br>5. Eleza jinsi Barnaba alikuwa mwenye bei kwake. Weka mkazo katika umuhimu wa kutia moyo katika maisha ya kikristo. Soma ***1 Samueli 30:6***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Baada ya kifo cha Stefano, wakristo walitawanyika, na wengine walikuja Antiokia.<br>2. Walihubiri habari njema ya Yesu na wengi waliamaini na walikuja kwa Yesu.<br>3. Barnaba alitumwa kutoka Yerusalema kwa ajili ya kusaidia wakristo wapya. Aliona ukubwa wa kazi na kwa hiyo alikuja pamoja na Saulo kule Antiokia muda wa mwaka mzima, walifundisha watu wengi katika Kanisa.<br>4. Wakati ule ule, Roho Mtakatifu aliamuru kanisa itume Barnaba na Saulo kwa ajili ya kazi mpya.<br>5. Walipanda chombo na Kwenda Kipuro kule walijikuta na upinzani wa mtu moja aliyeitwa Elema mchawi ambaye alijaribu kumzuiza Sergio Paulo, mtawala, kuwa mkristo. Saulo alimpinga Elema kwa nguvu, huyo alipigwa na upofu, na Sergio Paulo alimwamini Bwana Yesu.<br>6. Weka mkazo katika umuhimu wa kuhubiri neno katika kutangaza Injili. ***(Matendo 11:19-20)***.<br>7. Weka pia mkazo katika umuhimu wa kukomea kama mkristo ***(1 Petro 2:2)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | Zungumzieni kuhusu magumu ya maisha ya kikristo kupitia mfano wa Saulo. | 1. Kwa nini kazi ya Paulo na Barnaba ulifanikiwa? Fasilia jibu yako.<br>2. Mafundisho gani tunaweza kupata katika kukutana kwa Paulo na Elema, kuhusu nguvu ya Mungu juu ya pepo wabaya. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Wengine wanawaza kwamba maisha itakuwa pasipo magumu wakati wanaamini. Kulingana na wewe, ni shauri gani ambayo Paulo angepana kwa watu wanaowaza namna hii? Soma ***2 Wakorito 11:23-33***.<br>2. Andika maombi ya kuwatia moyo wakristo ambao wamejaribiwa. Fanya ma karatasi na uipane kwa mkristo ambaye unajua na eko katika magumu. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Ikiwezekana, leta nafasi kwa Watoto ili wakutane na muhubiri ao Pastori, na umuombe aeleze historia zingine za kuamini kwa mshangao ambako Aliona katika utumishi wake. Hiyo ilifanya tendo gani kwako?<br>2. Zungumza na kiongozi moja mkristo ambaye unajua kuhusu jinsi unaweza kuongeza uelewa wako wa Biblia na kutunga matengenezo yako mwenyewe ya usomaji wa Biblia. |

| | A9 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Muhubiri | A9 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Mtume Paulo<br>Kichwa – Mahubiri yake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 13:1-12***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 13:12***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Roho Mtakatifu alikuwa akifanya kazi na ujumbe wa Injili uliendela kutangazwa maeneo mengi.<br>2. Inawezekana kuwe upinzani wa Shetani juu ya injili. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 13:13-52***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 13:49***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ujumbe wa unabii kuhusu kuja kwa Kristo ulikuwa tangu zamani katika Agano la Kale, pia kufa kwake na kufufuka vilifanyika kabisa kulingana na mpango wa Mungu.<br>2. Usamee wa zambi unapatikana tu kupitia Bwana Yesu. |
| **KUTANGULIZA** | Tanguliza habari ya upinzani kati ya Mungu na Shetani. Anza maelezo tangu shamba la Edeni kisha zungumzieni pamoja kuhusu historia ya kuanguka. Kumbusha kwamba bado Shetani anaendelea kutenda kwa njia nyingi na kila mara anapinga Injili ya Bwana Yesu. | Uwaulize wanafunzi wafikirie kuhusu umuhimu wa usamee. Kumbukeni mambo inayofanyika katika maisha ya kila siku mule wanaweza kusamee mtu. Angalieni kwa sababu ya nini tunahitaji usamee wa Mungu. Onyesha jinsi Kristo eko katikati kabisa katika ujumbe wa kikristo wa usamee wa zambi. Chunguzeni mawazo ingine ya uwongo kuhusu usamee. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Baada ya kifo cha Stefano, wakristo walitawanyika, na wengine walikuja Antiokia.<br>2. Walihubiri habari njema ya Yesu na wengi waliamaini na walikuja kwa Yesu.<br>3. Barnaba alitumwa kutoka Yerusalema kwa ajili ya kusaidia wakristo wapya. Aliona ukubwa wa kazi na kwa hiyo alikuja pamoja na Saulo kule Antiokia muda wa mwaka mzima, walifundisha watu wengi katika Kanisa.<br>4. Wakati ule ule, Roho Mtakatifu aliamuru kanisa imtume Barnaba na Saulo kwa ajili ya kazi mpya.<br>5. Walipanda chombo na Kwenda Kipuro kule walijikuta na upinzani wa mtu moja aliyeitwa Elema mchawi ambaye alijaribu kumzuiza Sergio Paulo, mtawala, kuwa mkristo. Saulo alimpinga Elema kwa nguvu, huyo alipigwa na upofu, na Sergio Paulo alimwamini Bwana Yesu.<br>6. Saulo alimpinga Elema kwa nguvu, huyo alipigwa na upofu, na Sergio Paulo alimwamini Bwana Yesu.<br>7. *Zungumzieni pamoja kuhusu ukweli wa kushikwa na mapepo wachafu na jinsi inafanyika kwa njia tofauti.*<br>8. *Sema kuhusu umuhimu wa ujumbe wa Injili ule wakati pia wakati wa sasa.*<br>9. *Chunguzeni kwa sababu ya nini hukumu wa Mungu ulimuangukia Elema.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo amefika katika mji mwingine unaoitwa Antiokia (wa Pisidia).<br>2. Wakati wa ujumbe wake wa kwanza, anaeleza maneno yote kuhusu historia ya Wayuda na jambo kubwa iliyo kuja kwa Yesu, kufa kwake na ufufko. Kwa kumaliza, amesema kwamba “ni kupitia yeye ndio usamee wa zambi zenu umetangazwa”.<br>3. Baada ya huu ujumbe wa kwanza katika sunagogi, amealikwa kuja tena sabato iliyofuata.<br>4. Na siku ile, karibu mji wote ulikuja kumsikia Paulo; hiyo ilifanya kwamba viongozi wa Wayuda walipata wivu kabisa.<br>5. Paulo anawaambia kwamba kwa sababu walikataa Neno la Mungu, tangu sasa ataenda kwa mataifa, kama vile imesemwa katika ***Isaya 49:6***.<br>6. Eleza kwa nini viongozi wa wayuda walitaka kwamba Yesu afe.<br>7. Fikirini kuhusu sababu ya nini ilipaswa Yesu afe na namna kufa na kufufuka kwa Yesu ilikuwa katika mpango wa Mungu.<br>8. Angalia jinsi Yesu Mwokozi ni wa kipekee ***(angalia mistari 38-39)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | Uliza wanafunzi maswali kwa kuwasaidia kurudia na kushika vizuri somo hii. | Uliza wanafunzi maswali kwa kuwasaidia kurudia somo hii. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Linganisha jibu la Elema na ile ya Sergio Paulo mbele ya ujumbe wa Injili. Jibu ya wanafunzi wako wakati huu ni ya namna gani?<br>2. Ndani ya filamu nyingi wakati wa sasa, uchawi imetajwa humo kabisa (kwa mfano Harry Potter). Je, wakristo wanapaswa kuangalia filamu za namna hii? Zungumzieni jambo hili. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Namna gani asili ya Kristo ya kipekee kama Mwokozi ni changamoto kubwa katika tabia yetu?<br>2. Someni pamoja ***Waefeso 4:32*** kisha fikirini pamoja na wanafunzi juu ya tendo la maneno hii ya Paulo kuhusu usamee! |

| | A9 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Mji uliogawanyika | A9 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Mtume Paulo<br>Kichwa – Shida zake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Maendo 13:13-16; 42-52***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 13:49***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ni ya muhimu kusikia Neno la Mungu.<br>2. Ujumbe kuhusu Yesu ni kwa watu wote, na unaleta furaha kwa wale wanaupokea. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 14:1-28***<br>**Mstari muhimu:** ***Marko 16:20***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ujumbe wa Injili unatenganisha watu na wakati mwingine unaweza kusababisha hatari kali.<br>2. Uaminifu kwa Kristo, kama vile Paulo aliionyesha, ni ya muhimu kabisa. |
| **KUTANGULIZA** | Uwaulize wanafunzi kwa nini wanawaza kwamba Biblia ni ya muhimu kabisa. (Andika mara ngapi Neno la Mungu imetajwa katika usomaji wa Biblia).<br>Weka mkazo kabisa kwa wanafunzi wako katika wazo ya kwamba ujumbe wa Kristo uko katikati ya Biblia, na kwamba ujumbe huu unaelekea watu wote. Uwakumbushe kwamba katikati ya Wakristo, kuna tofauti kubwa kuhusu asili za kitamaduni. | Ambia wanafunzi walete maana ya neno “uaminifu”. Uwasaidie kupata mifano ya uaminifu katika maisha ya kila siku pia watu ambao wanaonyesha uaminifu. Kwa nini uaminifu ni ya muhimu kabisa? |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo amefika katika mji mwingine unaoitwa Antiokia (wa Pisidia).<br>2. Na siku ile, karibu mji wote ulikuja kumsikia Paulo; hiyo ilifanya kwamba viongozi wa Wayuda walipata wivu kabisa.<br>3. Paulo anawaambia kwamba kwa sababu walikataa Neno la Mungu, tangu sasa ataenda kwa mataifa, kama vile imesemwa katika Isaya 49:6.<br>4. *Amsha akili ya wanafunzi kuhusu kabila ya wale ambao walimsikia Paulo* ***(mistari 16, 42, 43, na 48)***.<br>5. *Eleza jinsi Neno la Mungu ilisambazwa.* ***(mstari 49)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Wakati Paulo na Barnaba walipofika hapo Ikonio, wayuda wengi na wasiowayuda wakaamini lakini Wayuda wengine walipinga.<br>2. Mji uligawanyika kwa sababu ya Injili. Wengine walitaka kumpiga mawe Paulo na Barnaba na kwa sababu ya hiyo, walikimbilia pale Listra.<br>3. Katika mji huu, Mungu anamtumia Paulo kwa kuponya mtu moja mwenye kupooza miguu. Wakaaji wa mji wanawaza kwamba Paulo na Barnaba ni miungu na wanataka kuwatolea sadaka.<br>4. Mitume hawa wawili wanaambia watu kwamba wanajaribu kuwaondosha kwenye sanamu zao isiyo ya faida ili wamtumikie Mungu aliye hai. Wanakumbusha kila kitu ambacho Mungu anatupatia ***(mstari 17)***.<br>5. Wayuda wanafika kutoka Antiokia na Ikonio na wanashawishi watu kumpiga Paulo mawe. Wanampeleka inje ya mji, ameonekana kabisa kwamba amekufa. Kwa bahati Paulo anaishi na siku iliyofuata, anaendelea na safari yake, pamoja na Barnaba, hadi Derbe. Wanafanya pale wingi fulani wa wanafunzi.<br>6. Kisha wanarudi kule Listra, Ikonio na Antiokia kwa ajili ya kutia wakristo moyo, ingawa hatari ambayo ilikuwa juu yao.<br>7. *Weka mstari katika tabia ya Mungu* ***(mistari 15-17)***.<br>8. *Angalia umuhimu wa kudumu, kwa mfano wa Paulo na Barnaba. Soma kwa usikilivu kabisa* ***mstari 22***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| **KUIMARISHA** | Uliza wanafunzi maswali kwa kuwasaidia kurudia na kushika vizuri somo hii. | Uliza wanafunzi maswali kwa kuwasaidia kurudia na kushika vizuri somo hii.<br>1. Shabaa ya “ma ishara na ajabu” katika ***mstari wa 3*** ilikuwa nini?<br>2. Kwako wewe, Paulo na Barnaba wanaenda mbali sana katiika uaminifu wao kwa Mungu katika mstari huu? Mungu anatarajia kwamba tutoe maisha yetu kwa ajili ya kazi yake? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Angalia jibu la wale wasiowayuda ku ujumbe kuhusu Bwana Yesu katika mistari ***42 na 48***. Ni nini tunaweza kujifunza katika hiyo kuhusu jibu letu sisi wenyewe ku ujumbe wa Injili?<br>2. Ulizeni kuhusu shirika moja la kimisionari kwa kuvumbua kwa njia gani wa misionari wanapeleka Injili katika tamaduni nyingine. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Ndani ya vikundi, ambia Watoto waandike maneno inayoanza na herufi zilizo katika neno “aminifu” wakichagua maneno ingine ambayo itawezesha kuelewa vizuri zaidi jinsi uaminifu unaweza kutendeka katika maisha ya mkristo.<br>2. Fanya kibao kubwa kwenye ukuta ambacho kitasaidia wanafunzi ili wafikili pamoja kuhusu nguvu ya Injili juu ya kuabudu sanamu katika dunia yetu ya leo. |

| | A10 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Paulo anateseka kwa ajili ya Bwana | A10 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Paulo katika Filipi |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 14:1-21***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Petro 4:16***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wakati mwingine wakristo wanateseka kwa sababu ya imani yao. Na hawapaswi kuacha wakati wa magumu.<br>2. Wakristo wanamwamini Mungu aliye hai ambaye ni muumbaji na anajibu mahitaji yetu yote. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 16:9-40***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 16:31***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ni ya muhimu kusikia na kutii uongozi wa Mungu.<br>2. Mungu ndiye anafungua moyo wa watu na wokovu ni kwa mtu yeyote anayemwamini Bwana Yesu Kristo. |
| **KUTANGULIZA** | Chunguzeni pamoja na wanafunzi kwa nini ni ya muhimu kumwamini Mungu muumbaji. Weka mkazo katika wazo la kwamba sisi tuna mzigo na tunapaswa kutoa hesabu kwa Mungu. | Uliza wanafunzi kwa nini sisi wote tunahitaji wokovu wa Mungu.<br>Eleza wokovu hii iko je na jinsi inatumika kwa njia ya kwamini ile Mungu alitimiza kupitia Bwana Yesu, na siyo kwa njia ya matendo yetu sisi wenyewe. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Wakati Paulo na Barnaba walipofika hapo Ikonio, Wayuda wengi na wasiowayuda wakaamini lakini Wayuda wengine walipinga.<br>2. Mji uligawanyika kwa sababu ya Injili. Wengine walitaka kumpiga mawe Paulo na Barnaba na kwa sababu ya hiyo, walikimbilia pale Listra.<br>3. Katika mji huu, Mungu anamtumia Paulo kwa kuponya mtu moja mwenye kupooza miguu. Wakaaji wa mji wanawaza kwamba Paulo na Barnaba ni miungu na wanataka kuwatolea sadaka.<br>4. Mitume hawa wawili wanaambia watu kwamba wanajaribu kuwaondosha kwenye sanamu zao isiyo ya faida ili wamtumikie Mungu aliye hai. Wanakumbusha kila kitu ambacho Mungu anatupatia ***(mstari 17)***.<br>5. Wayuda wanafika kutoka Antiokia na Ikonio na wanashawishi watu kumpiga Paulo mawe. Wanampeleka inje ya mji, ameonekana kabisa kwamba amekufa.<br>6. Kwa bahati, Paulo anaishi na siku iliyofuata, anaendelea na safari yake, pamoja na Barnaba, hadi Derbe.<br>7. Weka mstari katika tabia ya Mungu ***(mistari 15-17).***<br>8. *Angalia jinsi ni ya muhimu kudumu kama vile Paulo na Barnaba.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu alimuonyesha Paulo wazi kwamba hapaswi Kwenda katika eneo zingine za Asia, lakini alipata maono wakati wa usiku ikimuonyesha kwamba anapaswa kwenda katika Makedonia (Ulaya).<br>2. Eleza mambo iliyofanyika ili Injili ifike katika Ulaya ***(mstari 9)***.<br>3. Katika Filipi, Paulo alikutana na kundi la wanawake ambao walikuwa wakiomba pembeni ya mto. Mmoja wao aliitwa Ludia.<br>4. Eleza maana msemo “Bwana alifungua moyo wake” ***(mstari 14)***.<br>5. Wakati Paulo aliamuru pepo mchafu kutoka ndani ya binti moja mtumwa ambaye alikuwa na pepo ya kuagua, yeye na Sila walitupwa ndani ya kifungo.<br>6. Inchi ilitetemeka na wafungwa wote walijikuta huru. Mlinzi alikuwa karibu na kujiua lakini Paulo alimtuliza, akimwambia kwamba hakuna hata moja aliyekimbia.<br>7. Eleza kwa maneno iliyo mwepesi ulizo ya mlinzi na jibu la Paulo ***(mistari 30-31)***.<br>8. *Weka mkazo katika neno ya kwamba Bwana Yesu Kristo yupo Katikati kabisa kuhusu wokovu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| **KUIMARISHA** | Ambatanisha somo ya Biblia na Kutoka 20:1-6. Saidia wanafunzi kuelewa kwamba Mungu ni hai na ni kweli. Angalieni ni aina gani ya ma sanamu katika dunia yetu ya leo ambayo inaweza kutuzuiza kumpa Mungu pahali ambapo anastahili. | 1. Eleza ni nini ilifanyika baada ya kuamini kwa mlinzi.<br>2. Katika mstari huu, ubatizo ni nini? Inafanyika namna gani na kwa lazimisho gani? ***(mistari 15, 31-33)*** |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Wazeni pamoja kuhusu mzigo tunao mbele ya Mungu na magumu ya jambo ili kwetu. Hiyo inapaswa kuleta mabadiliko gani ndani ya maisha yetu ya ukristo?<br>2. ***Mstari 15*** inatufundisha nini kuhusu kuabudu “washujaa” fulani wa Biblia? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Saidia wanafunzi kushika ukweli wa kwamba wokovu inawezekana tu kwa neema ya Mungu.<br>2. Uwakumbushe umuhimu wa ubatizo kwa mkristo. |

| | A10 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Rafiki wa maisha | A10 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Mtume Paulo<br>Kichwa – Paulo katika Tesalonika na Beroya |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 16:1-3; 2 Timoteo 1:1-5***<br>**Mstari muhimu:** ***2 Timoteo 3:15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wakati tunasoma Maandiko, inatupatia akili hata tupate wokovu.<br>2. Ni ya muhimu kuwa na marafiki wakristo na kuombeana wamoja na wengine. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 17:1-14***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 17:11***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu ndiye Kristo, ambaye alitabiriwa katika Agano la Kale, na kifo chake na kufufuka vilikuwa vya lazima.<br>2. Ni ya muhimu kuchunguza Maandiko kwa kuelewa vizuri imani ya kikristo ni nini. |
| KUTANGULIZA | Zungumzieni pamoja kuhusu vitu ambavyo vinafanya tendo kabisa katika maisha yetu, ikiwe mu namna mzuri ao mbaya. Tia mkazo kuhusu umuhimu wa kupata vitu ambavyo vinatukokotea katika mwenendo bora wa kikristo ndani maisha yetu. Kumbuka watu ambao walifanya alama kubwa ndani ya imani yako na ilionekana namna gani. | Uliza wanafunzi watu wa muhimu sana kwao ni wa nani. Kwa nini mtu fulani ao mwingine ni wa muhimu? Eleza kwamba ujumbe wa kikristo ni kuhusu mtu moja wa kipekee. Uwaalike wasikie ujumbe huu jinsi umepewa katika ***Matendo 17:1-14***. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza kuhusu maisha ya familia ya Timoteo.<br>2. Eleza kazi kubwa ambayo mama yake na tata yake ya Timoteo walifanya kuhusu imani yake.<br>3. Fikirieni pamoja kuhusu umuhimu wa kutamani familia ya kikristo.<br>4. Chunguzeni kwa nini Paulo aliona kwamba ni ya muhimu kumutahiri Timoteo. Tunaweza kupata mafundisho gani katika hiyo.<br>5. Kisha, Timoteo alianza kusafiri pamoja na Paulo na alikuwa msaidizi wa muhimu.<br>6. Soma maneno ambayo Paulo anamwambia Timoteo ndani ya barua ambayo alimuandikia ***(2 Timothée 1:3-5)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo alisafiri kutoka Filipi kwenda Tesalonika kwenye alihubiri ndani ya sunagogi.<br>2. Eleza ujumbe ambao Paulo alihubiri ndani ya sunagogi pale Tesalonika. Eleza pia maana ya cheo “Kristo”, maana yake mjumbe wa Mungu, mpakaliwa wa Mungu, Mwokozi.<br>3. Angalieni matokeo ya ujumbe huu.<br>4. Fikirieni kuhusu maneno haya: “Watu hawa waliopindua dunia…” ***(mstari 6)***.<br>5. Paulo na Sila, mara tena, waliondoka usiku kwa haraka Kwenda katika Beroya.<br>6. Wayuda wa Beroya hawakuwe kabisa sawa wale wa Tesalonika, walikuwa wanachunguza Maandiko kila siku ***(mistari 11-12)***.<br>7. Lakini, kulionekana tena upinzani kubwa na ilibidi wandugu wamlazimishe Paulo aondoke. Walimpeleka hadi Atene.<br>8. Linganisha upinzani ambao Paulo na Sila walipata na ule ambao wakristo wengine wanapata siku hizi katika Imani yao.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | Mujifunze pamoja mstari muhimu kisha zungumzeni pamoja kuhusu jinsi imefanya muhtasari wa somo ya leo. | Soma ***Yosua 1:8*** kisha linganisha mstari huu na mstari muhimu ***(Matendo 17:11)***. *Ni magumu gani tunakuta humo juu yetu sisi, wakristo?* |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Saidia wanafunzi kuelewa jinsi ni ya muhimu kuwa na marafiki wakristo.<br>2. Tutatafuta namna gani urafiki na wakristo?<br>3. Onyesha umuhimu wa kuombea marafiki zetu vielvile memba za familia zetu ili wamwamini Bwana Yesu. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Juu ya kuhesabia Biblia kama msinghi wa maisha yetu, inapaswa kuisoma na kuijua (angalia mstari muhimu).<br>2. Wakati tunaamini kwamba Yesu ni mfalme, hiyo inapaswa kubadilisha maisha yetu. |

| | A10 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Paulo ndani ya kifungo | A10 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Mtume Paulo<br>Kichwa – Paulo katika Atene na Korinto |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 16:9-34***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 16:31***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wokovu unakuja kupitia Bwana Yesu.<br>2. Wale ambao wanaokolewa lazima wabatizwe. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 17:15-34; 18:1-18***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 17:30-31***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Kutubu ni agizo ambayo imepewa na Mungu.<br>2. Mungu atahukumu dunia. |
| **KUTANGULIZA** | Uwaelezee wanafunzi hadisi moja ya uokoaji. Uitumie kwa kueleza maana ya maneno “kuokolewa”, “Mwokozi” na “wokovu”. Uwatie moyo wale ambao wamekwisha kuokolewa washuhudie Imani yao mbele ya wanafunzi wengine ndani ya darasa. | Ambia Watoto waeleze maana ya kutubu. Uifanye kupitia ***1 Watesalonika 1:9*** ili ikusaidie. Unapoweka mkazo katika wazo la kumgeukia Mungu kama Mwokozi, eleza kwamba hiyo inabidi kuacha nyuma namna yako yako ya kuishi ya zamani. Kumbuka kuingiza humo ushuhuda za watu ambao walibadilishwa na Injili ili ukazishe maana ya kutubu. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza mambo iliyofanyika ili Injili ifike katika Ulaya ***(mstari 9)***.<br>2. Katika Filipi, Paulo alikutana na kundi la wanawake ambao walikuwa wakiomba pembeni ya mto. Mmoja wao aliitwa Ludia.<br>3. Eleza maana ya msemo “Bwana alifungua moyo wake” ***(mstari 14)***.<br>4. Wakati Paulo aliamuru pepo mchafu kutoka ndani ya binti moja mtumwa ambaye alikuwa na pepo ya kuagua, yeye na Sila walitupwa ndani ya kifungo.<br>5. Inchi ilitetemeka na wafungwa wote walijikuta huru. Mlinzi alikuwa karibu na kujiua lakini Paulo alimtuliza, akimwambia kwamba hakuna hata moja aliyekimbia.<br>6. Eleza kwa maneno iliyo mwepesi ulizo ya mlinzi na jibu la Paulo ***(mistari Matendo 16:30-31)***.<br>7. *Onyesha mamlaka iliyo katika jina la Yesu* ***(mstari 18)****.*<br>8. *Eleza kwamba wakati mwingine wakristo wanaweza kuteswa* ***(mstari 23)****.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo amefika hivi Atene na anaongojea marafiki zake wamfuate. Amehuzunika kabisa kwa kuona wingi wa sanamu katika mji ule.<br>2. Anaanza kuhubiri habari ya Yesu katika viwanja vya watu wote pia ndani ya sunagogi.<br>3. Paulo anapelekwa pahali pazuri (aeropago) kwenye ameombwa kueleza mafundisho hii mpya.<br>4. Paulo anasema kuhusu Mungu mkubwa muumbaji ambaye alifanya dunia, lakini anasema vilevile kwamba huyu Mungu si mbali na kila moja wetu. Anasema pia kwamba Mungu atahukumu dunia kupitia mtu ambaye alichagua, yule ambaye alifufua kutoka wafu.<br>5. Waliposikia kuhusu ufufuko, wengi wanamcheka, lakini wengine wanaamini. Baada ya wakati, kidogo, Paulo anaenda katika Korinto.<br>6. Kule anakutana na Prisila na Akila ambao wanakuwa wasaidizi wake. Anakaa miezi 18 pale Korinto kwenye watu wengi wanaamini.<br>7. Mungu anamtuliza Paulo; hakuna kitu kibaya kitampata katika Korinto.<br>8. Amsha akili ya wanafunzi juu ya mafundisho ya Paulo kuhusu Mungu katika ***Matendo 17:24-31***.<br>9. Fikirieni kuhusu hukumu unaokuja.<br>10. Angalieni majibu tofauti ya watu katika Atene na Korinto mbele ya ujumbe wa Paulo.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | Fanyeni pamoja kibao na mambo yote inayoweza kukumbusha historia ya Paulo na Sila katika Filipi. | Linganisha jinsi Paulo alifanya kwa kutangaza Injili katika Atene na katika Korinto. Unaona tofauti? Kwa nini? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Je, kila mwanafunzi amekwisha kupata wokovu katika Yesu Kristo?<br>2. Onyesha hatua inayofuata wokovu: Kufananishwa na Kristo mbele ya watu wengi kwa njia ya ubatizo. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Saidia wanafunzi washike umuhimu wa kutubu na hitaji ya mkristo ya kuacha kila mara zambi ili amkaribie Mungu.<br>2. Zungumzieni kuhusu kazi yetu ya kuambia watu wengine kuhusu Injili na hukumu unaokuja. |

| | A10 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Mji wa Atene | A10 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Mtume Paulo<br>Kichwa – Paulo katika Efeso |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 17:10-34***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 17:30***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu ni Mungu aliye hai ambaye aliumba dunia.<br>2. Mungu anaamuru watu wote watubu.<br>3. Mungu atahukumu dunia kwa haki. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 19:1-40***<br>**Mstari muhimu:** ***Waefeso 2:8-9***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Neno la Mungu na kazi yake vilisambazwa pale Efeso.<br>2. Jina la Bwana Yesu lilitukuzwa. |
| KUTANGULIZA | Uliza wanafunzi neno “sanamu” ina maana gani kwao. Zungumza nao kuhusu amri mbili za kwanza katika ***Kutoka 20***. Tumia ***1 Watesalonika 1:9*** *ili ueleze maana ya kutubu.* | Rudieni pamoja masomo ambayo mulijifunza katika Majifunzo 3. Fikilini kuhusu toba na na inaweza kumaanisha nini katika maisha ya kila siku. Tia mkazo katika mawazo ya kwamba kila mara toba inakwenda pamoja na kubadilika kwa maisha.<br>Zungumzieni kuhusu ***Matendo 19:18-20***. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo amefika hivi Atene na anaongojea marafiki zake wamfuate. Amehuzunika kabisa kwa kuona wingi wa sanamu katika mji ule.<br>2. Anaanza kuhubiri habari ya Yesu katika viwanja vya watu wote pia ndani ya sunagogi.<br>3. Paulo anapelekwa pahali pazuri (aeropago) kwenye ameombwa kueleza mafundisho hii mpya.<br>4. Paulo anasema kuhusu Mungu mkubwa muumbaji ambaye alifanya dunia, lakini anasema vilevile kwamba huyu Mungu si mbali na kila moja wetu. Anasema pia kwamba Mungu atahukumu dunia kupitia mtu ambaye alichagua, yule ambaye alifufua kutoka wafu.<br>5. Waliposikia kuhusu ufufuko, wengi wanamcheka, lakini wengine wanaamini. Baada ya muda kidogo,, Paulo anaenda katika Korinto.<br>6. *Weka mkazo katika mambo ambayo Paulo alifundisha kuhusu Mungu* ***(mistari 24-31)***<br>7. *Kaza kusema kuhusu umuhimu wa ufufuko wa Yesu* ***(mstari 31)***.<br>8. *Zungumzeni kuhusu majibu tofauti kwa mahubiri ya Paulo* ***(mistari 32-34)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo anaendelea katika safari yake hadi Efeso kule anakutana na wanafunzi wegine ambao hawakupokea Roho Mtakatifu.<br>2. Eleza kwa nini ilikuwa ya muhimu kwamba Paulo abatize wanafunzi wa Yoane.<br>3. Kisha Wayuda wa sunagogi kukataa mara tena mahubiri ya Paulo, anafundisha wanafunzi ndani ya shule moja kwa muda wa miaka mbili.<br>4. Mungu anafanya miujiza ya ajabu kupitia Paulo ***(mstari 11)***. Watu wengi wanaamini na wanakiri Imani yao wazi kwa kuona uwezo wa Roho Mtakatifu kupitia Paulo. Eleza kile watu hawa walifanya ***(mstari 19)***.<br>5. Eleza kwa ufupi mambo ambayo ilisababisha watu wengi wakusanyike kule Efeso ***(mistari 23-40)***.<br>6. Eleza maana ya “ufalme wa Mungu” ***(mstari 8)***.<br>7. Eleza jinsi Neno la Mungu ilifanya alama kubwa kule Efeso ***(mstari 20)***.<br>8. *Eleza jinsi ni ya muhimu kwa mkristo mpya kuacha zowezo na matendo yake ya zamani.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | Katika kundi, fikilini jinsi ya kuhubiri Injili mu namna inayofaa. Munaweza kuendeleza Mawazo hii kwa kupanga kazi ya mahubiri ya Injili. | Andikeni pamoja taarifa ya habari kuhusu mambo ambayo ilifanyika katika ***Matendo 19***. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Toba ya kibinafsi. Inamaanisha nini kuacha zambi na kumgeukia Mungu?<br>2. Kuhubiri Injili. Tunaweza kugawana namna gani ujumbe wa Injili? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Imani ya kiksto inaitwa pia “njia” ***(mstari 9)***. Maana yake ni nini? Ina changamoto gani kwetu?<br>2. Tunaweza kupata mafundisho gani ya Kutenda sisi kama wanainchi, kutoka katika tendo la katibu wa mji jinsi ilivyoelezwa katika ***mistari 35 hadi 41***? |

| | A11 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Kugawana na wengine | A11 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Kusambishwa kwa Paulo<br>Kichwa – Yerusalema na Kundi la watu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 18:1-11***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 18:9-10***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Popote alipoenda, Paulo alitangaza kwamba Yesu ndiye Kristo.<br>2. Mungu alikuwa pamoja na Paulo na alimtia moyo kupitia maono. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 21:17-40; 22:1-30***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 22:14-15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Kisha kukatazwa katika hekalu, Paulo alitoa ushuhuda kwa watu wengi.<br>2. Wayuda walichukia tendo la kwamba wasio wayuda walipokea na kuleta jibu ku Injili.<br>3. Paulo alikumbusha kwamba yeye ni mwanainchi wa kiroma wakati ambao alikuwa karibu kupigwa fimbo. |
| **KUTANGULIZA** | Uwaelezee watoto historia yako kibinafsi inayoonyesha mfano wa jinsi Mungu alikutia nguvu katika maisha yako. Zungumzeni kuhusu umuhimu wa kujitia nguvu katika maisha ya ukristo. Ambia wanafunzi walete mifano ya hiyo katika maisha yao wenyewe. | Eleza kwa ufupi upinzani ambao Paulo alipata alipofika katika Yerusalema.<br>Tumia tovu la "Sauti la waliokufa juu ya Imani" (ao njia zingine sawa ile) ili ulete mifano ya wakristo ambao walitoa ushuhuda wa Kristo kwa ujasiri na hawakuogope mateso. Uliza wanafunzi kwa nini mkristo anafanya vile? |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo anafika kule Korinto kwenye anakutana na Prisila na Akila ambao wanakuwa wasaidizi wake.<br>2. Kulingana na zoezo yake? Paulo anaingia kila siku ya sabato katika sunagogi ili awahakikishie Wayuda kwamba kweli Yesu ndiye Masiya ambaye wanaongojea.<br>3. Alipopingwa na Wayuda, alienda katika nyumba iliyokuwa pembeni na kuwahubiri wasio wayuda. Wengi wanaamini na kubatizwa.<br>4. Mungu anamtuliza Paulo; hakuna kitu kibaya kitampata katika mji huu wa Korinto na atamlinda katika mabaya yote ***(mstari 9)***. *Eleza kwamba hiyo ilimtia Paulo moyo kabisa.*<br>5. *Tia mkazo kwa kuonyesha jinsi Paulo alisambaza ujumbe* ***(mistari 4 na 11)***.<br>6. *Angalieni jinsi Neno la Mungu ilisambazwa pale Korinto. Tia mkazo katika umuhimu wa ubatizo.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo anafika Yerusalema na kwenda katika hekalu. Ameshitakiwa kwamba anaingiza huko mtu asiye myuda. Hiyo inasababisha fujo.<br>2. Kamanda wa kiroma anakuja kusaidia na kumpa nafasi ya kusema mbele ya watu wengi akisimama katika ngazi za ngome.<br>3. Paulo anaweza kujitetea na kushuhudia wazi ***(Matendo 22:1-21)***. Wakati aliposema kwamba Mungu anamtuma kwa wasiowayuda, hiyo inasababisha tena fujo ingine.<br>4. Wanampeleka katika ngome na kamanda anataka kumsambisha kwa kumpiga fimbo lakini Paulo anasema kwamba yeye ni mroma na hawezi kusambishwa kwa fimbo na anaweza kupigwa ila tu ikiwa anaonekana kuwa na kosa.<br>5. *Tia mkazo kuhusu juu ya nini Paulo alienda katika hekalu.*<br>6. *Eleza kabisa mambo ambayo ilifanyika wakati wa kuamini kwa Paulo.*<br>7. *Eleza kwa nini watu walimpinga kabisa Paulo.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| **KUIMARISHA** | Rudia somo hii kupitia michezo. | Ongoza mazungumzo kuhusu kuamua kwa Paulo aende katika hekalu kule Yerusalema. Alikuwa na sheria kwa kufanya vile? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Soma ***Zaburi 23*** kisha fikirieni kuhusu ahadi ya uwepo wa Mungu inatutia moyo sisi kama wakristo.<br>2. Tafuteni pamoja matendo ambayo munaweza kutumia kwa kutia moyo watu wengine kwa kupitiza wakati pamoja nao. Jaribu kuitenda. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Wakristo wanafungwa kila siku duniani. Fanyeni mpango wa maombi mara kwa mara kwa ajili ya kuombea wakristo wanateswa .<br>2. Uwaambie wanafunzi wafikili juu ya wiki iliyopita na kufikili kuhusu nafasi ile "ilipita" ambayo walikosa kutoa ushuhuda wa Kristo. Uwaambie watafute msaada wa Mungu juu ya ujasiri na uaminifu katika ushuhuda wao. |

| | A11 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Shauri juu ya uzima wake | A11 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Kusambishwa kwa Paulo<br>Kichwa – Kaisaria na watawala |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 23:10-24; 24:22-27***<br>**Mstari muhimu:** ***Zaburi 18:31***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu alimtia moyo Paulo wakati Wayuda walitaka kumuua.<br>2. Paulo aliendelea kuhubiri Neno la Mungu kwa uaminifu, hata wakati alikuwa mfungwa. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 23:23-26; 24:1-27; 25:1-12***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Petro 3:15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wanampeleka Paulo kwenye Kaisaria juu ya kumkinga na mwishowe anaomba kuhukumiwa na Kaisari.<br>2. Kila mara katika kusambishwa kwa Paulo, alihubiri haki, kujizuiza pia kuhumu unaokuja ***(24:25)***. |
| KUTANGULIZA | Kumbusha nguvu ya ufalme wa kiroma wakati wa Paulo. Eleza ngabo ni nini. Jaribu kupata picha za ulimwengu wa zamani wa wayunani na waroma na askari wa kiroma aliye na ngabo. Eleza jinsi Bwana ni ngabo ya watu wake.<br>Uwaambie watoto wajifunze mstari muhimu: ***Zaburi 18:31***. | Eleza historia ya Martin Luther na msimamo wake kwa ajili ya Kristo wakati wa mkusanyiko, ambao ulifanyika katika mji wa Worms mwaka wa 1521. Fikilini kuhusu mambo ambayo Martin Luther alisema wakati ule: … “Isipokuwa nikihakikishiwa kosa langu kwa msingi wa Maandiko ao kwa sababu zilizo wazi ... zamiri yangu imefungwa na Neno la Mungu.” Tumia hii kama kingilio kwa kueleza mambo ambayo Paulo aliishi. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo anapelekwa mbele ya baraza ya kidini ya Wayuda.<br>2. Mabishano inaamshwa wakati Paulo anasema mambo ya ufufuko. Hakika, wamoja wanaamini na wengine wanakataa kuamini, na inasababisha kelele kubwa ***(23:9)***.<br>3. Uzima wa Paulo uko katika hatari na anaokolewa na kamanda wa kiroma.<br>4. Usiku ule, Bwana anamuonekania Paulo na anamwambia ajitie moyo kwa sababu ataenda hadi Roma kwa ajili ya kutangaza ujumbe wa Injili.<br>5. Wayuda wengine wanajitoa ili wasikule wala kunywa kabla ya kumuua Paulo, na wanafanya shauri kuhusu kusudi hiyo.<br>6. Kwa bahati, mwipwa wa Paulo anasikia mazungumzo hii, na anamwambia kamanda ambaye alimkinga Paulo na huyo anafanya kwamba aondoke katika salama Kwenda katika Kaisaria.<br>7. Kisha, Paulo anasambishwa mbele ya Feliki mtawala wa kiroma, na mara tena, anaweza kueleza Injili.<br>8. *Weka mkazo katika ujumbe ambao Paulo alihubiri kwa Feliki na umuhimu wake leo.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo anapelekwa Kaisaria kwa ajili ya ulinzi wake mwenyewe na anaonyeshwa mbele ya mtawala Feliki.<br>2. Kisha, anasambishwa mbele yake na wakati huu viongozi wa wayuda wanamshitaki kwamba anakufuru hekalu na anataka kuleta fujo.<br>3. Paulo anajitetea na baadaye anazungumza tena na Feliki na kueleza wazi kuhsu Imani katika Yesu Kristo ***(24:24)***.<br>4. Paulo anakaa miaka mbili katika kifungo, hadi kuchaguliwa kwa mtawala mpya.<br>5. Anasamba mbele ya huyo (Festo), na mara tena, viongozi wa wayuda weko pale kwa ajili ya kumshitaki. Paulo anakataa Kwenda Yesrusalema juu ya kuhukumiwa na anaomba kuhukumiwa na Kaisari. Festo anaruhusu aende katika Roma.<br>6. *Zungumzeni kuhusu jinsi Paulo anajitetea mbele ya Feliki.*<br>7. *Unawaza, kwa nini Feliki aliogopa wakati aliposikia mahubiri ya Paulo? **(24:25)**.*<br>8. *Kwa nini Paulo aliomba kuhukumiwa na Kaisari, na matokeo yake ni nini?*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | Andika mambo ambayo Paulo angeandika katika gazeti yake na kichwa cha neno: “Kuongojea ahadi ya Mungu.” | Andika kwa mchanganyiko ao chora katika kibao ao karatasi kubwa mawazo yako kuhusu majifunzo hii, katika Kichwa cha neno “Msimamo wa Paulo kwa ajili ya Yesu Kristo.” |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Waza kuhusu ahadi ambayo Mungu alimpa Paulo usiku. Je, kuna kitu fulani ao mtu ambaye aliweza kuzuiza kutimilika kwa ahadi hii? Namna gani jambo hii inaweza kututia moyo leo?<br>2. Felikji alitetemeka na kuogopa kwa kusikia Neno la Mungu ***(Matendo 24:25)***. Je, inatufikia kwamba tunatetemeka mbele ya Neno la Mungu? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Soma ***2 Timoteo 2:3***. Fanya daftari ya magumu ambayo ulipata kwa sababu ya imani yako. Andika pembeni namna Mungu alikutia moyo na kukusaidia wakati ule wa majaribu.<br>2. Paulo alitumia hali yake kama mwanainchi wa kiroma. Kwa ajili ya maendeleo ya Injili. Tunaweza kutumia jinsi gani faida tunazo kwa kusambaza Injili? |

| | A11 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Mbele ya mfalme | A11 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Kuhukumiwa kwa Paulo<br>Kichwa – Kaisaria na mfalme |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 25:13-22; 26:13-32***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 26:22***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Paulo alipaswa kusambishwa mbele ya Festo.<br>2. Mfalme Agripa alikuwa karibu kuwa mkristo. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 25:13-27; 26:1-32***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 26:28***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anatenda kwa faida ya Paulo. Festo anaamua kwamba asistahili hastahili kifo, na Agripa anawaza kwamba anaweza kuachiliwa.<br>2. Paulo alitangaza wazi ujumbe wa Injili na alitaka kumkokota Agripa awe mkristo. |
| **KUTANGULIZA** | Uliza wanafunzi kwamba anaweza kuwa mkristo namna gani. Eleza kwamba hii haiwezi kufanyika kwa lazimisho, lakini tia mkazo katika umuhimu wa kuhakikishia watu ili waamini. Chukua mifano katika maisha yako mwenyewe inayoonyesha kwamba wakati mwingine tunaweza kulazimishwa kufanya kitu fulani ao kingine pasipo kuhakikishwa. | Zungumzieni kuhusu aina za upinzani ambao tunaweza kukutana nao kwa sababu ya Imani yetu ya kikristo. Wanafunzi wanaweza kufanya namna gani? Fikilini kuhusu ahadi ambayo Bwana Yesu alifanya kwa wanafunzi katika ***Luka 21:12-15***. Ahadi hizi imetimilika namna gani katika majifunzo ya leo? |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Kunapita miaka mbili tangu Paulo anajikuta katika kifungo. Sasa, Festo ndiye mtawala mpya. Wayuda walitaka kumpeleka Paulo kule Yerusalema ili ahukumiwe kule, lakini Paulo alitaka kuhukumiwa na Kaisari katika Roma.<br>2. Mfalme Agripa na mke wake Berenika wanafika Kaisaria na wanataka kujua zaidi kuhusu Paulo mfungwa.<br>3. Sasa Paulo anahukumiwa mbele ya Agripa.<br>4. Paulo anaeleza ushuhuda wake mwenyewe ***(26:1-23)***.<br>5. Festo anamwambia kwamba ana wazimu! Agripa anasema kwamba sasa hvi Paulo anataka kumkokota awe mkristo. Wote wawili wanakubaliana kwamba Paulo alipaswa kuachiliwa lakini kwa sababu alitaka kuhukumiwa na Kaisari, inapaswa aende kule Roma.<br>6. Tia mkazo katika utetezi wa Paulo mbele ya Festo, na uamuzi wake. ***(26:24-25)***. Chunguza pia jinsi gani Paulo alitafuta kumkokota Agripa awe mkristo.<br>7. Waza pia kuhusu jibu la Paulo mbele ya kukiri kwa Agripa. ***(26:29)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Kunapita miaka mbili tangu Paulo anajikuta katika kifungo. Sasa, Festo ndiye mtawala mpya. Wayuda walitaka kumpeleka Paulo kule Yerusalema ili ahukumiwe kule, lakini Paulo alitaka kuhukumiwa na Kaisari katika Roma.<br>2. Mfalme Agripa na mke wake Berenika wanafika Kaisaria na wanataka kujua zaidi kuhusu Paulo mfungwa.<br>3. Sasa Paulo anahukumiwa mbele ya Agripa.<br>4. Paulo anaeleza ushuhuda wake mwenyewe ***(26:1-23)***.<br>5. Festo anamwambia kwamba ana wazimu! Agripa anasema kwamba sasa hvi Paulo anataka kumkokota awe mkristo. Wote wawili wanakubaliana kwamba Paulo alipaswa kuachiliwa lakini kwa sababu alitaka kuhukumiwa na Kaisari, inapaswa aende kule Roma.<br>6. *Tia mkazo katika utetezi wa Paulo mbele ya Festo, na uamuzi wake.* ***(26:24-25)****. Chunguza pia jinsi gani Paulo alitafuta kumkokota Agripa awe mkristo.*<br>7. Waza pia kuhusu jibu la Paulo mbele ya kukiri kwa Agripa. ***(26:29)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | Fanyeni pamoja kibao moja na maneno hii: “Kuhakikishiwa Karibuni tu?” | Fikilini kuhusu majifunzo hii mukichunguza maana ya misemo ifuatatayo: “Ni mzuri zaidi kuhakikishiwa kuliko Kutenda kwa kulazimishwa.” Mapatano gani iko kati ya sentensi hii na na kile tunajifunza katika majifunzo hii? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tunajisikia je kwa kuona jinsi Paulo alihubiri Injili? Kuna vitu ambavyo tunaweza kuiga.<br>2. Fanyeni mfano wa mazungumzo mule mwanafunzi moja anajaribu kuvuta mwingine ili awe mkristo. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Linganisha mtazamo wa viongozi Wayuda na Waroma mbele ya Injili katika kitabu cha Matendo. Mafundisho gani tunaweza kupata kuhusu majibu tofauti ambayo tunaweza kukuta siku hizi mbele ya Injili?<br>2. Ni magumu gani munaona kuhusu njia tofauti ambayo tunaweza kutumia kwa kutangaza Injili? |

| | A11 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maisha ya Paulo<br>Kichwa – Kuzama | A11 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Kuhukumiwa kwa Paulo<br>Kichwa – Kuzama katika bahari ya Mediteranea |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 27:13-14, 20-44; 28:1-9***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 27:25***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu ameahidi kutusaidia katika kila hali tunayojikuta ndani ya maisha.<br>2. Mipango ya Mungu inatimilika kila mara. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 27:1-44; 28:1-10; 28-31***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 27:24-25***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anatawala mambo yote mule tunajikuta, na anaahidi kutusaidia ili tuishinde.<br>2. Tendo ya kwamba watu wengine wanakataa Injili inawawezesha wengine kuisikia. |
| KUTANGULIZA | Uliza watoto kama wamekwisha kujikuta katika zoruba. Walijisikia namna gani wakati ule? Waliomba kwamba Mungu awaokoe? Tengeneza mazingira ambayo itawezesha kuambatanisha mambo haya ambayo wanafunzi waliishi na kuzama kwa Paulo. | Zungumza pamoja na wanafunzi kuhusu woga. Uwaambie waseme ni kitu gani ambacho wanaogopa kabisa. Fikilini kuhusu umuhimu wa ahadi za Mungu katika mambo ya namna hii ***(Psaumes 23:4)***. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo anajikuta ndani ya chombo akielekea Roma. Anawashauri wafanya kazi wasiendelee kusafiri na chombo wakati wa baridi, lakini hakuna mtu ambaye alimsikia.<br>2. Zoruba kubwa inatukia na inadumu siku nyingi. Siku moja usiku, Paulo anapata maono mule Mungu anamfunulia kwamba wote watafika salama kwenye inchi kavu. Sasa anawaambia kwamba anamwamini Mungu na mambo yote itafanyika jinsi aliambiwa.<br>3. Mwishowe wanaweza kukaribia Melita na wanasimamisha chombo. Wasafiri 276 wanashuka katika udongo, wote salama!<br>4. Wakaaji wa Melita wanaonyesha wema wao kwa watu hawa, na Paulo anatenda miujiza nyingi katika kisanga kile.<br>5. *Onyesha jinsi Mungu alimsaidia Paulo na kumtia moyo wakati wa zoruba.*<br>6. *Uwaeleweshe wanafunzi kwamba wakristo wanapaswa kuishi nyakati za magumu kama vile kila mtu.*<br>7. *Fikilini kuhusu ukweli wa kwamba wakati tunapopata zoruba katika maisha, tunaweza kuishi uwepo na nguvu ya Mungu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Paulo anajikuta ndani ya chombo akielekea Roma. Safari hadi Krete inafanyika kwa magumu na Paulo anawashauri wafanya kazi wasiendelee kusafiri na chombo wakati wa baridi, lakini hakuna mtu ambaye alimsikia.<br>2. Zoruba kubwa inatukia na inadumu siku nyingi. Wafanya kazi wanapoteza tumaini yote ya kuweza kuokolewa.<br>3. Siku moja usiku, Paulo anapata maono mule Mungu anamfunulia kwamba wote watafika salama kwenye inchi kavu. Sasa anawaambia kwamba anamwamini Mungu na mambo yote itafanyika jinsi aliambiwa. Baada ya masiku kumi na ine pasipo kula kitu, Paulo anawatia moyo wakule. Baada ya muda mfupi, wanaona pwani.<br>3. Mwishowe wanaweza kukaribia Melita na wanasimamisha chombo. Wasafiri 276 wanashuka katika udongo, wote salama!<br>4. Wakaaji wa Melita wanaonyesha wema wao kwa watu hawa, na Paulo anatenda miujiza nyingi katika kisanga kile.<br>5. Mwishowe wanafika Roma kwenye Paul anawekwa chini ya kifungo cha nyumbani lakini anatumia kila bahati kuwaambia watu kuhusu Bwana Yesu.<br>6. *Onyesha jinsi Mungu alimsaidia Paulo na kumtia moyo wakati wa zoruba.*<br>7. *Uwaeleweshe wanafunzi kwamba wakristo wanapaswa kuishi nyakati za magumu kama vile kila mtu.*<br>8. *Fikilini kuhusu ukweli wa kwamba wakati tunapopata zoruba katika maisha, tunaweza kuishi uwepo na nguvu ya Mungu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | Ambia wanafunzi wajiweke pahali pa Paulo na wataandikia barua rafiki, moja ambaye anajikuta katika magumu. Wataeleza ndani ya barua hii jinsi Mungu aliwalinda wakati wa zoruba walipokuwa wakienda ku Roma. Wanafunzi watatumia mfano huu kwa kumtia rafiki moyo. | Soma ***2 Wakorinto 11:21-33 na 2 Timoteo 4:16-18***.<br>Zungumzieni kuhusu mapatano iliyo, kati ya mashairi hii mbili. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Historia ya Paulo ya kuzama inatufundisha namna gani? Inatutia moyo?<br>2. Tunaweza kupata mafundisho gani katika historia nyingine za Biblia mule Mungu anaokoa watu (Yosefu, Danieli,…) wakati wa magumu?<br>3. Andika maombi ya kushukuru kwa kumsifu Mungu juu utawala wake kubwa katika maisha yetu. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Fikilini kuhusu mambo mbalimbali ya maisha ya Paulo ambayo mulijifunza. Kumbuka ni kwa kiasi gani tunaona humo uaminifu wa Mungu.<br>2. Tafuta katika kamusi maana ya neno “kudumu”. Tunaiona namna gani ndani maisha ya Paulo? Uwasaidie wanafunzi kufikili juu ya kudumu kwao wenyewe, zaidi kwa kuilinganisha na ile ya Paulo. |

| | **A12 – KIWANGO 3**<br>**Somo 1 – Krismasi ya kwanza**<br>**Kichwa – Haiwezekani** | **A12 – KIWANGO 4**<br>**Majifunzo 1 – Kuzaliwa kwa Mwokozi**<br>**Kichwa – Ujumbe wa malaika** |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 1:5-20; 57-66***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 1:37***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Zakaria na Elizabeti walikuwa wanadoa wazee na waliona Mungu anajibu maombi yao.<br>2. Hakuna kisichowezekana kwa Mungu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 1:18-25; Luka 1:36-38***<br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 1:21***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Kuzaliwa kwa Yesu kulitabiriwa vizuri na malaika ambaye alimfunulia yule ambaye atakuwa baba yake maelezo ya muhimu kuhusu maisha yake.<br>2. Malaika alimuonekania pia Maria, akimuonyesha kwamba atachukua mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. |
| **KUTANGULIZA** | Zungumzieni ukweli wa kwamba wakati mwingine inapaswa kuongojea ili kuona Mungu ajibu maombi yetu. Eleza hali ya Zakaria na Elizabeti ambao waliongojea muda mrefu jibu ya maombi yao! Ile ilionekana kwao kwamba haiwezekani! | Fikilini kuhusu njia za mawasiliano za wakati wetu ambayo inawezesha kupeleka habari duniani pote kwa haraka. Lakini, hakuna mtu anayeweza kusema kabisa mambo itakayofanyika kabla itimilike! Mungu pekee anaweza kuifanya! Yosefu na Maria, wote wawili, walipata ujumbe kutoka kwa Mungu kuhusu kuzaliwa kwa Bwana Yesu, kabla ifike. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza kwamba Zakaria na Elizabeti walitaka kufanya familia. *Onyesha haya na maumivu ambayo inatukia sababu ya kukosa mtoto katika jamaa wakati ule, katika mashariki.*<br>2. Zakaria, katika kazi yake kama kuhani, alikuwa na bahati ya kutumika ndani ya hekalu.<br>3. Malaika anamtokea na anaogopa. Malaika huyu anamwambia kwamba Elizabeti atapata Mwana ambaye atakuwa mkubwa mbele ya Bwana na atatayarisha watu walioandaliwa kwa ajili ya Bwana.<br>4. Zakaria anasema kwamba wao ni wazee sana kwa kupata watoto. Malaika anamjibu kwamba, kwa sababu asiamini Neno la Bwana, atabaki bubu hadi siku itakapofanyika.<br>5. Mtoto alipozaliwa, Elizabeti anasema kwamba ataitwa kwa jina la Yoane, na Zakaria anahakikisha jina hii kwa kuandika. Mara moja, anaweza tena kusema. Anajazwa na Roho Mtakatifu na anatabiri kuhusu mambo yote ambayo mwana wake atafanya.<br>6. *Angalieni jibu ya majirani na ya wakaaji wote wa kandokando **(Luka 1:65-66)**.*<br>7. *Kumbukeni tofauti iliyo kati ya jibu la Elizabeti ku ujumbe wa malaika na ile ya mume wake. Tunaweza kupata mafundisho gani kwa hiyo?*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Maria na Yosefu walikuwa wachumba. Kisha Maria anapata ujumbe wa Malaika, ikimuelezea kwamba atazaa Mwana, ambaye atachukuliwa katika mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.<br>2. Wakati Yosefu alipojua mambo hii, anataka kuachana naye kwa siri. Lakini, malaika anamwambia katika ndoto, kuhusu kuzaliwa kwa mtoto huyo, kuhusu sababu ya jambo ile pia kuhusu unabii ambao utatimilika wakati ule.<br>3. Yosefu na Maria waliamini wote wawili ujumbe ambao waliambiwa, na kulingana na agizo ambayo walipata, Yosefu anampa mtoto jina la Yesu, “kwa sababu ndiye atakayeokoa watu wake toka zambi zao”. (Matayo 1:21).<br>4. *Angalieni maswali hii tatu:*<br>*a. Kwa nini Yesu alichukuliwa katika mimba kwa muujiza na siyo mu namna ya kawaida?*<br>*b. Kwa nini Yosefu na Maria walichaguliwa ili wawe wazazi wake duniani? (Angalia daftari ya mababu zao katika **Matayo 1 na Luka 3**).*<br>*c. Kwa nini Mungu alichagua kumtuma Mwana wake wa pekee duniani?*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| **KUIMARISHA** | Tengeneza karatasi kubwa kisha uandike Kichwa cha neno hiki: “Isiyowezekana inawezekana”. ambia wanafunzi waandika mambo ambayo ilifanyika (zaidi mifano ya kutoka katika Biblia), hata kama ilionekana kuwa haiwezekane. Andika chini ya karatasi “Aksanti Mungu!” | Ni mambo gani ambayo inaambatana na maisha yako ambayo unaweza kushika katika majifunzo hii? Kulingana na wewe, kuja kwa Bwana Yesu kuna maana gani? Tayarisha maombi ya kushukuru kwa ajili ya kila kitu ambacho Mungu alifanya kwa kumtuma mwana wake ***(2 Wakorinto 9:15)***. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Unajifunza nini kwa upekee kupitia somo hii?<br>2. Unawaza kwamba inawezekana kuona malaika siku hizi? Kwa sababu ya nini ndio na kwa sababu ya nini hapana? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Je, Mungu amekwisha kutangaza kitu fulani, kwako wewe ao kwa mtu unayejua, ambacho kilionekana kuwa nguvu kuamini?<br>2. Onyesha matabiri katika usomaji wa Biblia ambayo ilitimilika wakati Bwana Yesu alikuja. |

| | A12 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Krismasi ya kwanza<br>Kichwa – Kazi ya upekee | A12 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Kuzaliwa kwa Mwokozi<br>Kichwa – Agizo ya mfalme |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 1:26-38***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 1:38***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Maria na Yosefu walikuwa wanandoa wa kipekee, walitumiwa na Mungu mu namna ya pekee kabisa.<br>2. Kuzaliwa kwa Yesu, Mwana wa Mungu, ilikuwa muujiza. | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 2:1-7***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 2:7***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wafalme wa ufalme wa kiroma waliitwa Kaisari.<br>2. Amri moja ya Kaisari huyo, Augusto, ilimlazimisha Maria na Yosefu kusafiri hadi Betelehemu juu ya kujiandikisha. Kwa hiyo, wametimiza unabii wa Agano la Kale. |
| **KUTANGULIZA** | Zungumzieni kuhusu hitaji ya kupana jina kwa mtoto mara moja baada ya kuzaliwa. Yesu alikuwa na majina mengi na ma cheo. Tafuta pia onyesha kati ya hiyo katika historia ya ***Luka 1 na 2 na Matayo 1 na 2***. Uliza wanafunzi wanapendelea historia gani na ni juu ya nini? | Katika vikundi kidogo, onyesha maeneo tofauti ambayo imetajwa katika usomaji wa Biblia. Fanya vivyo, hivyo kuhusu majina ya watu. Angalia kuwa hausahau chochote wakati unaposoma tena maandiko. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Pengine Maria angali kijana na amechumbiwa na Yosefu<br>2. Anatembelewa na Malaika Gabrieli. Anashangaa kwa kujua kwamba Mungu anampa neema ya kipekee.<br>3. Malaika anamwambia kwamba atazaa mtoto atakayeitwa kwa jina la Yesu. Yeye ni Mwana wake Mungu aliye juu na atampa kiti cha baba yake Daudi.<br>4. Maria anachanganyikiwa, kwa sababu bado anagali bikira lakini malakika anamuelezea kwamba mtoto atachukuliwa katika mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.<br>5. Kwa sasa jibu ya Maria haishangaze sana! Anasema: “Iwe kwangu sawa na neno lako”<br>6. Fikilini pamoja kuhusu mawazo yote ambayo iliweza kuwa katika akili ya Maria wakati Malaika alimwambia kwamba amepata neema na bila kukawia atachukua mimba. Angalia pia ***mistari 46 na 47***.<br>7. “Hakuna kisichowezekana kwa Mungu.” Kumbukeni watoto wengine ndani ya Biblia ambao walizaliwa jinsi isiyowezekana kwa binadamu.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Maria na Yosefu wote wawili walikuwa wa kizazi cha mfalme Daudi. Ndiyo maana walienda hadi Betelehemu wakati kwandikisha majina kuliamuriwa.<br>2. Ilikuwa safari ya kilomita karibu 110 na ilikuwa magumu sana kwa Maria ambaye alikuwa karibu kuzala. Bila shaka mji wa Betelehemu ulikuwa mwenye kujaa na Yosefu na Maria walikaa katika aina moja ya zizi ao pango.<br>3. Ni pale ambapo Yesu alizaliwa katika mazingira ya umasikini na unyenyekevu.<br>4. *Tazameni mambo yote ambayo ilifanyika ili Yesu azaliwe katika Betelehemu, kama vile Mika alivyosema. Mushangazwe na uwezo wa Mungu aliyetimiza haya yote* ***(Mika 5:2)***.<br>5. *Soma* ***Yoane 3:16*** *na* ***Wagalatia 4:4****. Fikilini kuhusu maana ya mistari hii ili usaidie kila mmoja aelewe maana ya hii tukio kubwa.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| **KUIMARISHA** | Jibu maswali ifuatayo:<br>1. Malaika yule aliitwa namna gani?<br>2. Kwanza, Maria alifanya nini kuhusu habari hii.<br>3. Alijisikia namna gani baadaye? ***(mistari 46-47)*** | Jibu maswali ifuatayo:<br>1. Leta jina ya mji fulani ambao ulikuwa ku kilomita 110 kutoka kwenye wewe unaishi.<br>2.Je, wanafunzi wangetamani kutembea hivi kwa miguu, katika, hali ya mwisho wa mimba?<br>3. Onyesha tofautri kati ya kuzaliwa kwa Yesu na kuzaliwa siku za leo. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Katika vikundi kidogo, onyesha maeneo tofauti ambayo imetajwa katika usomaji wa Biblia. Fanya vivyo hivyo kuhusu majina ya watu. Angalia kuwa hausahau chochote wakati unaposoma maandiko. Fikilini kuhusu umuhimu wa kila kitu ambacho muliandika. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Andika sentensi kidogo sawa ikiwa wewe ni Yosefu. Hii ndio kichwa cha neno cha historia yake: “Maria, mwisho wa mimba, anasafiri urefu wa kilomita 110 kabla ya kumzala mtoto yetu ambaye aliwekwa katika sanduku ya kulisha nyama” |

| | A12 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Krismasi ya kwanza<br>Kichwa – Huko Betelehemu | A12 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Kuzaliwa kwa Mwokozi<br>Kichwa – Kutembelewa na wachungaji |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 2:1-20***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 2:11***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mpango wa Mungu ulikuwa kwamba Yesu azaliwe katika mazingira ya umasikini na ya magumu.<br>2. Mungu alikuwa anatawala kila kitu ambacho kilifanyika wakati ule, na anatawala kila kitu siku hizi pia. | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 2:8-20***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 2:11***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Malaika aliwatokea wachungaji ambao walikuwa wakifanya kazi yao ya kila siku.<br>2. Waliamini mambo waliosikia, na walitenda kutokana na hiyo pasipo kusita. |
| **KUTANGULIZA** | Ambia wanafunzi wataje mambo makuu ambayo ilifanyika katika historia. Eleza kwamba kuja kwa Mwana wa Mungu duniani ni tukio moja kubwa. Chora mpangilio wa matukio mwenye imepangwa tukio zote za somo hii. | Katika vikundi kidogo onyesheni historia kwa mfano wa mchezo. Chukueni vitu vyepesi kama kipande cha nguo iwe sawa kitambaa cha wachungaji. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Maria na Yosefu wote wawili walikuwa wa kizazi cha mfalme Daudi. Ndiyo maana walienda hadi Betelehemu wakati kwandikisha majina kuliamuriwa.<br>2. Ilikuwa safari ya kilomita karibu 110 na ilikuwa magumu sana kwa Maria ambaye alikuwa karibu kuzala. Bila shaka mji wa Betelehemu ulikuwa mwenye kujaa na Yosefu na Maria walikaa katika aina moja ya zizi ao pango.<br>3. Ni ambapo alizaliwa katika mazingira ya umasikini na unyenyekevu.<br>4. Tunawaza kwamba kuzaliwa huku ilikuwa usiku na wachungaji walikuwa wanakesha wakati watu wengi walikuwa wamelala.<br>5. Walipata habari ya kuzaliwa kwa Mwokozi, ambaye ni Masiya, Bwana.<br>6. Kundi la malaika wa jeshi la mbingu waliomsifu Mungu waliwaonekania wachungaji.<br>7. Wachungaji waliamua Kwenda hadi Betelehemu kwa ajili ya kuona ni nini ambayo ilifika.<br>8. Walieleza kandokando yao mambo yote ambayo waliona na kisha walirudi wakishangilia utukufu wa Mungu.<br>9. *Fikiria salamu ya kwanza ya Malaika hapa kama vile pahali pengine ndani ya Biblia.*<br>10. *Waza jinsi wanandoa hawa wapya walijisikia muda wa safari.*<br>11. *Ni mafundisho gani inaweza kushikwa katika hii historia ya wachungaji?*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Tunawaza kwamba kuzaliwa huku ilikuwa usiku na wachungaji walikuwa wanakesha wakati watu wengi walikuwa wamelala.<br>2. Walipata habari ya kuzaliwa kwa Mwokozi, ambaye ni Masiya, Bwana.<br>3. Kundi la malaika wa jeshi la mbingu waliomsifu Mungu waliwaonekania wachungaji.<br>4. Wachungaji waliamua kwenda hadi Betelehemu ili waone ni nini ambayo ilifanyika. Walikuta kule Maria, Yosefu na mtoto, kama walivyoambiwa.<br>5. Walieleza kandokando yao mambo yote ambayo waliona na kisha walirudi wakishangilia utukufu wa Mungu.<br>6. *Fikilini kwamba Mungu aliwatokea watu hawa kwa njia ya malaika wakati walikuwa wakifanya kazi. Anaweza pia kusema nasi leo wakati tunahusika na kazi yetu ya kila siku.*<br>7. *Wakati tunaposikia kile Mungu alifanya kwa ajili yetu, tunapaswa kwambia watu wengine.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | Jibu maswali ifuatayo:<br>1. Unawaza, kwa nini Malaika wanasalimia watu kama vile katika ***mstari 10***?<br>2. Unawaza kwamba siku hizi Mungu anasema kupitia malika kwa watu wa kawaida sawa wachungaji? Sababu ya nini ao sababu ya nini sivyo?<br>3. Ni vitu gani Maria aliwaza ndani ya moyo wake, kulingana na wewe? ***(mstari)*** | Jibu maswali ifuatayo:<br>1. Unawaza, kwa nini wachungaji walitenda kwa haraka kabisa baada ya Kwenda kwa Malaika?<br>2. Mungu alibariki wachungaji kwa sababu walitenda pasipo kukawia. Unaweza kuandika ***mstari 20*** na maneno ya leo?<br>3. Kulingana na wewe, Maria alikuwa anawaza nini katika moyo wake? ***(mstari 19)*** |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Fikiria ikiwa wewe ni mmoja wa wachungaji. Ukitumia ***mistari 8 hadi 17***, Andika ndani ya "gazeti" yako mambo ambayo ulisikia, kuona na kujisikia. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Kwa nini hauwezi kwanza gazeti mule utaandika vitu ambavyo Mungu alikwambia na tarehe, ili upate kuwangalia nyuma na kuona kile ambacho Mungu anafanya katika maisha yako. Hiyo itakutia moyo! |

| | A12 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Krismasi ya kwanza<br>Kichwa – Katika hekalu | A12 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Kuzaliwa kwa Mwokozi<br>Kichwa – Zawadi za waakili |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 2:22:40***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 2:30***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Simioni na Ana walifurahi sababu ya kuzaliwa kwa Yesu kwa maana walielewa bei yake.<br>2. Ni yamuhimu kumshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu duniani. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 2:1-23***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 2:11***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ingawa waakili walileta ma hazina, hazina ya kweli, ni Yesu mwenyewe.<br>2. Watu hawa walielewa kwamba Yesu ni mtu wa upekee kabisa. |
| **KUTANGULIZA** | Fikilini kuhusu furaha kubwa inayotukia wakati wa kuzaliwa kwa mtoto. Ni nini ilikuwa tofauti katika kuzaliwa kwa Yesu? Eleza kwamba sheria ya kiyuda ililazimisha kwamba wazazi waende katika hekalu kwa ajili ya kumpa mtoto jina, juu ya kumtahiri, na juu ya kutoa sadaka kwa ajili ya utakaso wa mama na kwa ajili ya kumshukuru Mungu (Walawi 15). | Fikilini kuhusu furaha kubwa inayotukia wakati wa kuzaliwa kwa mtoto. Kumbukeni kuja kwa familia na marafiki kwa ajili ya kumuona mtoto huyu. Eleza kuhusu waakili na safari ya mrefu. Kumbukeni ukweli wa kwamba ndani ya historia hii, kila mara Mungu alikuwa amekwisha kumtangulia Shetani. Fanya daftari ya mifano ya hiyo katika maandiko haya. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Muda mfupi baada ya kuzaliwa, Yesu anapelekwa na wazazi wake katika hekalu hapo Yerusalema.<br>2. Maria na Yosefu wamekwisha kujua kwamba inapaswa kumpa mtoto wao jina la Yesu, na wanafanya vile! Kisha, wanatoa sadaka kulingana na sheria.<br>3. Wanakutana na Simioni, ambaye alitambua, kupitia Roho Mtakatifu, kwamba hatakufa kabla ya kumuona “Masiya wa Bwana”.<br>4. Anamchukua mtoto mikononi mwake na anamshukuru Mungu kwa sababu anatambua kwamba Yesu ndiye Mwokozi.<br>5. Maria na Yosefu wanakutana pia na mzee mwanamke aliyeitwa Ana. Naye pia, anamshukuru Mungu na anasema “habari ya Yesu kwa wote ambao walikuwa wanaongojea ukombozi katika Yerusalema.”<br>6. *Fikilini kuhusu jambo ya kwamba Simioni na Ana walijua wote wawili kwamba Yesu alikuwa mtu wa upekee kabisa.*<br>7. *Fikilieni kuhusu kila kitu ambacho walisema kuhusu Yesu na kuhusu mambo ambayo itamfikia.* ***(Angalia mistari 31-32, 34-35 na 38.)***<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Waakili wanaona nyota mpya katika mashariki na kulingana na majifunzo yao, wanaelewa kwamba mfalme mpya amezaliwa sasa hivi. Wanataka Kwenda kumkuta kwa ajili ya kumwabudu.<br>2. Wanafika hadi kwa Herode katika nyumba yake ya kifalme kule Yerusalema, wakizani kwamba mfalme mpya atakuwa kule.<br>3. Herode anafazaika kwa sababu anaogopa mpinzani. Lakini walimu wa sheria wanaamsha akili yake kuhusu unabii wa ***Mika 5:1*** unaotabiri kuzaliwa kwa mfalme huyu katika Betelehemu.<br>4. Sasa waakili wanaendelea na safari yao hadi Betelehemu, wanakuta mtoto wanamtolea hazina zao na wanamwabudu.<br>5. Walipoonywa katika ndoto, wanarudi katika inchi yao kwa njia ingine, na hawamwabie kitu Herode.<br>6. Malaika anamwambia Yosefu amchukue Maria na mtoto katika Misri juu ya kuwalinda.<br>7. Herode anatambua kwamba waakili walimdanganya na anatuma waue Watoto wote wa umri wa chini ya miaka mbili katika Betelehemu na katika eneo yake yote.<br>8. Mwishowe, alipoonywa katika ndoto, Yosefu anasikia kwamba anaweza kurudi kwa salama kuishi katika Israeli. Sasa anakuja kuishi katika Nazareti pamoja na Maria na Yesu.<br>9. *Fikilini kuhusu mpango wa Mungu tangu mia za miaka pia kuhusu matabiri tofauti.* ***(Angalia mistari 5-6, 17-18, 23.)***<br>10. *Kumbuka pia kwamba Herode alifanya kazi ya Shetani.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| **KUIMARISHA** | Simioni anasema kwamba Yesu atakuwa nuru. Katika vikundi kidogo, fikilini kuhusu faida ya nuru. Namna gani Mawazo hii inaweza kusaidia wanafunzi kuelewa vizuri zaidi ***mstari 32***?<br>Uwatie wanafunzi moyo wamuombe Mungu atume nuru zaidi katika maisha yao. Uwasaidie kutaja maeneo kwa upekee mule wanahitaji msaada, na muifanye kuwa hitaji ya kuombea. | Chukueni muda kwa kufikili kuhusu ma zawadi ambayo ilitolewa kwa Yesu. Zahabu kwa ajili ya mfalme, uvumba kwa ajili ya Mwokozi ambaye atateseka na kufa, na manemane kwa ajili ya Mungu, yule ambaye tunaabudu.<br>Angalieni jinsi Yesu ni kama hazina, zawadi ya bure kwa yeyote anayempokea kama Mwokozi na Bwana. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Wewe ulijifunza nini kibinafsi katika somo hii?<br>2. Waza kwamba wokovu inaleta mabadiliko ya umutu wetu wote na mwendo unaodumu muda wa maisha yetu yote. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Ni zawadi gani tunaweza kuleta kwa Bwana Yesu?<br>2. Fanya daftari ya mifano katika maisha ya kila siku mule tunaona Shetani akijionyesha kama “mdanganyifu”. Tambua nia zake. |

## Mashauri kwa wakufunzi wa masomo

**KIWANGO 3 (Masomo)**

- Wanafunzi watahitaji Biblia kwa kujaza masomo hii. Kwa kweli, watapaswa kutafuta shairi moja ao nyingi.
- Maswali iko na ma namna tofauti, kama mchezo wa maneno, visanduku vya maneno, maneno inayokosekana, na kazalika.
- Masomo imetungwa ili itumiwe na Biblia ya utafsiri wa Swahili ya Congo. Mistari ambayo imetajwa imetoshwa katika utafsiri huu.
- Shabaa ni kwamba, kila mwanafunzi, ingawa Biblia yake, aweze kujibu maswali ya masomo.
- Ma pointi 20 imepewa kwa wiki, na jumla ya ma pointi 80 kwa mwezi, ikiwa majibu yote ni ya kweli.
- Kwa jumla, pointi moja inapewa kwa kila jibu ya kweli, kama ilivyoonyeshwa pembeni ya kila kazi ndani ya kitabu.

**KIWANGO 4 (Majifunzo)**

- Majifunzo hii ina maelezo nyingi kuliko masomo ya kiwango cha 3.
- Ile inaonekana katika maswali magumu na majibu.
- Ma pointi 20 imepewa kwa wiki, na jumla ya ma pointi 80 kwa mwezi, ikiwa majibu yote ni ya kweli na kamili.

**NAMNA GANI KUREKEBISHA MASOMO?**

- Kuangalia kila ukurasa kwa kuchunguza majibu.
- Kuleta ma pointi kulingana na majibu.
- Kutumia kalamu ya rangi tofauti na ile mtoto alitumia.
- Kuongeza, ikiwa ni lazima, jibu inayofaa na kurekebisha makosa ya herufi (lakini hiyo haiwezi kupunguza kiwango cha pointi).
- Kupatia ma pointi kidogo kwa jibu isiyo ya kutosha kabisa ao ya kipande.
- Kuhesabu jumla ya ma pointi kwa mwezi na kuiandika katika ukurasa wa mwisho, pahali palipowekewa.

Ni ya muhimu kuwa mwema katika namna ya kupana ma pointi na kufanya yote iwezekanayo kwa kuwatia moyo watoto katika majifunzo yao ya Biblia. Usisite kusema neno ya kutia moyo, sifa, katika sanduku iliyopangwa kwa hoyo ukiandika kwa mfano rangi ilipakwa mzuri, usafi wa kazi, ma pointi iliyopewa, uelewa muzuri wa somo, na kazalika. Ni ya muhimu kwa mwanafunzi kuwa mwangalifu kweli ili a tofautishe uchunguzi. Maswali, maoni, misemo ya kutia moyo inaamsha akili ya mtoto. Lakini, kama ni misemo hiyo moja inarudiwa mara kwa mara, kwa wepesi itapoteza bei yake.

**KIWANGO 3**

**Maoni kwa jumla:**

“Kazi nzuri! Inaonekana kwamba ulisoma maswali na usikilivu. Zaidi nilipendezwa na jibu lakoi ku ile ya mwisho; ulifasilia muzuri!”

“Jambo Jonathan. Aksanti kwa kazi yako nzuri. Ni mzuri sana kwa kuwa unapata majibu yote. Nilikamilisha ile ilikosekana.”

**Maoni ya kiroho:**

“Musa aliishi mambo magumu na watoto wa Israeli, lakini Mungu hakumwache kushindana nao pekee.”

“Yosefu hajasahau kamwe kwamba baba yake alimfundisha kupenda Mungu. Aliikumbuka hata wakati alikuwa mbali na nyumbani.”

“Bartimayo aliamua kufika hata kwa Bwana Yesu. Hakukate tamaa, kwa sababu baadaye, aliweza kuona, na alijua kwamba Yesu alikuwa mtu wa kipekee.”

**KIWANGO 4**

**Maoni kwa jumla:**

“Mara tena Kazi mzuri sana! Inaonekana kwamba ulielewa vizuri mafundisho hii na ninawaza kwamba ilikupendeza. Aksanti kwa kuchukua muda kwa ajili ya kujibu na utaratibu wote. Ingekuwa raisi kuifanya kwa haraka, nimependezwa na namna yako ya kutumik!”

“Ulifanya nguvu, Rakeli. Nawaza kwamba, kulingana na majibu yako, haukuelewa mambo yote katika mafundisho hii. Pengine unaweza kuisoma mara tena?”

**Maoni ya kiroho:**

“Wakati mwingine imesemwa kwamba mifano ni historia za hapa dunia inayo na maana ya mbingu. Je, unafika kupata maana kamili, ao ya mbingu, ya mfano ulio katika Somo 3?”

“Stefano alipata kifo kibaya, lakini hakuwe na woga wa kufa, kwa sababu alijua kwamba Mungu aliongoza kila kitu, na atakuwa pamoja na Bwana Yesu mbinguni.”

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Congo-Swahili   SWC

11/2025